# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumamosi Septemba 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580350

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710







## Wafanyabiashara vigogo wa madini washikiliwa tuhuma kufanya magendo

UKURASA 3

UKURASA 11

# CCM yatangazia kiama wapinzani




**YASEMA** imeandaa makombora kuanika madudu yao lala salama, Polepole asema yakianza kupigwa watasambaratika... *Endelea uk. 2*



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi (kushoto), akionyesha kitabu chenye jina la Nasaha 10 kuelekea uchaguzi mkuu wa rais, wabunge, wawakilishi na madiwani, baada ya kukizindua jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mtunzi wa kitabu hicho, Sheikh Mohamed Iddi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Hussein Afif. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wataka Magufuli awatumbue Ma-DED waliokata wagombea

UKURASA 2



John Shibuda

## MWALIMU MBARONI TUHUMA RUSHWA YA NGONO

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, AZAM VITA YA KILELENI LIGI KUU LEO** UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Jaji Mmilla afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Bethuel Mmilla, amefariki dunia.

Taarifa ya Mtendaji wa Mahakama ya Rufani, Solanus Nyimbi, iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari ilisema Jaji Mmila alifariki dunia juzi katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Muhimbili jijini Dar es Salaam. Awali alilazwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo Septemba 23, mwaka huu alikokuwa akipatiwa matibabu.

Jaji Mmilla alizaliwa Septemba 22, 1956 katika Wilaya ya Makete mkoani Njombe na mwaka 1964 hadi 1970 alisoma shule ya Msingi Iniho wilayani Makete kabla ya kujiunga na Shule ya Sekondari Luigalo mkoani Iringa mwaka 1971 hadi 1974 na kuhitimu kidato cha nne.

Mwaka 1975 hadi 1976 aliendelea na elimu ya kidato cha tano na cha sita katika Shule ya Sekondari ya Ilboru mkoani Arusha kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1980 hadi 1983 kwa masomo ya shahada ya kwanza ya sheria (LLB).

Baada ya hapo, taarifa ilieleza kuwa aliajiriwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) Machi 21, 1978 ambako alifanya kazi hadi mwaka 1980 na mwaka 1983 alifanya kazi Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Mnamo Februari 1984, Jaji Mmilla aliajiriwa na Mahakama ya Tanzania katika nafasi ya Hakimu Mkazi ambako alifanya kazi katika vituo mbalimbali hadi Aprili, 1995.

Akiwa ndani ya Mahakama aliteuliwa pia kushika nafasi ya usajili kazi aliyoifanya hadi Juni, 2000 alipoteuliwa kuwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria hadi Juni, 2002.

Juni 05, 2002 aliteuliwa na Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, marehemu kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania nafasi ambayo aliitumikia mpaka Oktoba, 2012 alipoteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani hadi umauti unamfika.

Tarifa ilieleza kuwa msiba uko nyumbani kwa marehemu, Mikocheni jijini Dar es Salaam na mipango ya mazishi itajulikana baadaye.

Bwana alitoa, Bwana ametwaa, jina na Bwana lihimidiwe.

# CCM yaandaa makombora mazito

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema siku za mwisho za kumaliza kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kitatoa kile kilichokiita makombora mazito dhidi ya vyama vya upinzani.

Kimesema siku sita za mwisho kumalizia kampeni hizo, kitatoa siri nzito za wapinzani ambazo Watanzania watabaki wakipigwa na butwaa.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, alitoa ahadi hiyo jana mjini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya kampeni za uchaguzi walizofanya kwa muda wa wiki mbili.

"Upinzani wana mambo ya kutisha sana, tunasubiri tupige kubwa wakae chini, siku hiyo watu watashangaa. Ikifika Oktoba 23, 24, 25, 26, 27 itakuwa ni balaa... tukiyasema hapa itakuwa ni aibu. Kuna wabunge wa upinzani wanaunga mkono CCM maongezi yao tunayo, na hata leo (jana) kwenye vikao vyao tutakuwa nao," alisema Polepole.

Alisema awamu inayofuata ya kampeni, CCM itatumia mbinu za kimedani za kisiasa ambazo zitawamaliza wapinzani na kuwasambaratisha.

**USHIRIKIANO UPINZANI**

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Polepole pia alizungumzia ushirikiano unaotarajiwa kufanywa na vyama vya ACT-Wazalendo na CHADEMA katika uchaguzi huo, akisema wanasubiri kwa hamu muungano wa vyama hivyo vya upinzani.

"Tutawachapa mapema asubuhi wakiwa wameunga hivyo hivyo, nami ninatoa rai hawa wasisubiri tarehe tatu (Oktoba 3, mwaka huu) kuungana, hawa waungane 'from now' (kutoka sasa), ndipo watajua tulipotoka na Watanzania miaka mitano iliyopita na hapa tulipofika.

"Tumewekeza katika taifa hili nchi ikiwa maskini, Rais Magufuli amepambana na kuifikisha uchumi wa kati, tulitakiwa kufika mwaka 2025, lakini tumewahi kufika mapema," alitamba Polepole.

Polepole alikumbusha kuwa vyama vya siasa vya upinzani viliwahi kuungana miaka mitano iliyopita kupitia Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), lakini vikaambulia kipigo kutoka kwa Rais John Magufuli.

Kuhusu mwenendo wa kampeni za CCM tangu walipoanza hadi sasa, Polepole alisema wanaendelea vizuri na kuwaomba Watanzania kumchagua Dk. Magufuli kwa kishindo kwa kuwa hatawaangusha. "Tangu tumeanza kampeni tumekuwa tukiwatuma makada waandamizi sehemu mbalimbali, tunaendelea vizuri katika kampeni za majimbo, kata na urais. "Zanzibar tunaendelea vizuri sana, Dk. Hussein Mwinyi anaendelea kufanya mikutano sehemu mbalimbali. Tunachowaahidi Watanzania ni maendeleo ya haraka chini ya Dk. Magufuli na Dk. Mwinyi," alisema.

Aliongeza kuwa mgombea urais Dk. Magufuli amepata mapokezi makubwa katika mikoa yote aliyopita wakati akifanya kampeni ikiwamo Kagera, Kigoma, Geita, Singida, Tabora, Simiyu, Shinyanga na Mwanza.

**TUME YA UCHAGUZI**

Vilevile, Polepole alizungumzia suala la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwaengua wagombea baada ya kuwekewa mapingamizi, akidai kuwa ni mchakato uliofanyika kwa mujibu wa sheria.

Alisema wastani wa wagombea wa upinzani walioenguliwa ni 160 ambao hawakuwa na sifa wala vigezo.

Polepole alisema: "Kwa mfano, Jimbo la Ubungo, mgombea wa CHADEMA alipouliza unatokea mkoa gani akajaza DSM, mawakili wetu wakauliza DSM ndiyo nini? Tukampiga pingamizi. Tukaenda Jimbo la Ilamba Magharibi, mbunge wa upinzani alitakiwa kugonga mhuri wa Katibu wa Wilaya husika katika jimbo, yeye akagonga mhuri wa katibu wake. Tunampigia pingamizi.

"Baada ya hapo tukaisikiliza tume. Tume imewapendelea wale watu kwa zaidi ya asilimia 80. Tungesema tusimamie sheria na katiba, wale wagombea 160 wasingeshiriki uchaguzi. Tume imewarudisha wagombea 120 wa upinzani kwa huruma, sisi tumetulia, wamebakizwa 30 ambao hawajarudishwa, wanapiga kelele hadi Umoja wa Ulaya," Polepole alitamba.



Mgombea Mwenza wa Kiti cha Rais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika eneo la Meatu Stendi, Jimbo la Meatu, mkoani Simiyu juzi. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Wataka ma-DED waliokata wagombea watumbuliwe

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, John Shibuda, amemwomba Rais John Magufuli kuwatumbua wasimamizi wasaidizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), waliohusika kuenguliwa wagombea ubunge na udiwani katika mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi huo, wakurugenzi wa halmashauri (ma-DED) ndiyo wanakuwa wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu kuenguliwa kwa wagombea, Shibuda alisema amefanya ufuatiliaji kama mwenyekiti wa baraza hilo na kubaini NEC huamua kutokana na taarifa za maelekezo zinazotoka ngazi za chini.

"Rais Magufuli nikuombe kwa heshima, wasimamizi wasaidizi wa tume ya uchaguzi wanaochafua ahadi yako ya kuwapo kwa uchaguzi wa huru na haki, ninakuomba Mheshimiwa Rais chukua hatua za kuwatumbua, ili watu wajifunze, waache tabia za unafiki na uzandiki wa kupotosha na kuipaka matope serikali na Rais," alishauri.

Shibuda alisema NEC haina kitengo cha upelelezi, hiyo haina uhakiki kwa hujuma zinazofanywa ngazi ya chini na kupelekwa kwao.

Shibuda alisema anaamini Rais Magufuli hajatuma watu wazushe na kuidanganya tume ili kufanya uamuzi batili.

"Hili nimelisema kwa sababu nimelifanyia uchambuzi. Hata mimi kuna wagombea kupitia chama changu wameenguliwa kwa mizengwe," alisema.

**UKAWA MPYA**

Akizungumzia kusudio la baadhi ya vyama vya siasa kutaka kushirikiana katika uchaguzi huo, Shibuda alisema wanasiasa wana uchokozi wa kifikra kwa sababu vyama vyote vinaelewa sheria na kanuni zinasema nini kuhusu kuungana.

"Ninacheka kwa sababu hawajanishirikisha wala kuja kuomba ushauri kwangu, hilo ninadhani hebu tuliache lijitokeze, siyo kila mtoto wa kike akikutwa na mvulana basi ni mhuni," alisema.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, vyama vinne (CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD) viliungana na kusimamisha mgombea mmoja wa urais kupitia umoja ulioitwa UKAWA (Umoja wa Katiba ya Wananchi).

Mwaka huu, vyama viwili vya upinzani; ACT-Wazalendo na CHADEMA viko katika hatua za mwisho za kukubaliana kushirikiana katika uchaguzi huo licha ya kila kimoja kusimamisha mgombea kwenye nafasi ya urais.

**UKATA WA VYAMA**

Shibuda pia alisema vipo vyama vinavyopata ruzuku na vingine havipati, akibainisha kuwa hali ya uchumi ni mbaya na kinachofanyika kwa sasa ni kutembeza bakuli.

"Wale wenye ukata ni kweli wana ukata na hawawezi kulumbana na Msajili wa Vyama vya Siasa, afanyeje Msajili? Hana mafungu kwa sababu sheria tuliipitisha wenyewe na sheria ya mabadiliko ya kwamba vyama vyote visiwe vinapewa ruzuku ilitokana na wadau wa vyama vya siasa," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu Mkuu mbaroni tuhuma rushwa ya ngono

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), inamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyeregete iliyoko wilayani Mbarali mkoani Mbeya, Adelhard Mjingo (44), kwa tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mwanafunzi wake wa darasa la saba mwenye umri wa miaka 14 kwa ahadi kuwa angemsaidia kufaulu mitihani.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa jana, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema mwalimu huyo alinaswa na makachero wa taasisi hiyo Septemba 23, mwaka huu akiwa na mwanafunzi huyo kwenye moja ya nyumba za kulala wageni jijini.

Alisema taasisi hiyo ilipata taarifa za siri kutoka kwa mmoja wa wananchi kuwa mwalimu huyo amekuwa akiomba rushwa ya ngono kwa mwanafunzi wake huyo, akimtishia kuwa endapo angekataa, angehakikisha anamfelisha kwenye mtihani wake wa mwisho.

Matechi alisema kuwa siku ya tukio, mwalimu huyo aliaga shuleni kuwa anakwenda kwenye semina ya chanjo katika Mji wa Rujewa wilayani humo na aliondoka pamoja na walimu wenzake, lakini alipofika kwenye ukumbi wa semina, aliandikisha jina na kuomba udhuru kisha akaondoka.

Alisema Makachero wa TAKUKURU walibaini kuwa wakati mwalimu huyo anaondoka shuleni, alimtaka mwanafunzi wake huyo aondoke shuleni na kwenda nyumbani kubadili nguo, ili asijulikane kuwa ni mwanafunzi na akamtaka avae sweta lenye rangi nyekundu kama ishara ya kutambulika kwa dereva bodaboda aliyekuwa ameandaliwa kwenda kumchukua.

"Alimwelekeza mwanafunzi huyo kuwa akishabadilisha nguo, aende akasimame eneo la kibaoni, atamtuma mwendesha bodaboda aende kumchukua kumpeleka eneo watakalokutana," alisema.

Matechi aliongeza kuwa mwalimu huyo alichukua chumba kwenye nyumba ya kulala wageni (jina tunalihifadhi) iliyoko Rujewa na kisha akamtuma dereva bodaboda kwenda kumchukua binti huyo na alipofika, mwalimu alimpokea na kuingia naye chumbani.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema mwalimu huyo baada ya kuingia na mwanafunzi huyo chumbani, alimuuliza kama amekula na alipojibiwa kuwa hajala, alitoka na kwenda kumnunulia chipsi na soda kisha akaingia tena chumbani kwa ajili ya kutimiza azma yake.

Alisema kuwa wakati mwalimu huyo akijiandaa kutekeleza uhalifu huo, makachero wa TAKUKURU waliokuwa wanafuatilia tukio hilo, waliingia na kumweka chini ya ulinzi mwalimu huyo.

"Tunaendelea na uchunguzi wa tuhuma hizi, unaendelea kwa mujibu wa sheria na baada ya kukamilika, hatua zitachukuliwa dhidi ya mwalimu huyo ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani," alisema Matechi.

Alisema kukamatwa kwa mwalimu huyo ni matunda ya uanzishwaji wa klabu za wapinga rushwa shuleni na vyuoni pamoja na kampeni ya 'Vunja Ukimya Kataa Rushwa ya Ngono'.

Alisema kampeni hiyo inaendelea kutolewa kwa vijana ili wawe na ujasiri wa kukataa rushwa ya ngono kwa kutoa taarifa na kuwa sehemu ya mapambano dhidi ya rushwa.

Matechi aliwashukuru wananchi wanaoendelea kushirikiana na TAKUKURU kutoa taarifa za vitendo vya rushwa na viashiria vya vitendo hivyo. Aliwataka viongozi wote wenye dhamana kwenye ofisi mbalimbali ambao wanahudumia jamii, kuacha kutumia vibaya ofisi zao kwa kushawishi ama kuomba rushwa ya ngono kama kigezo cha kutoa huduma. Alisema Ofisi za TAKUKURU ziko katika kila wilaya na hivyo wananchi wanatakiwa kuzitumia kutoa taarifa ama kupiga simu namba 113 ama kutuma ujumbe mfupi kwenye namba hiyo au kubonyeza namba *113# na kufuata maelezo na kwamba huduma hiyo ni bure.

# Vigogo biashara madini washikiliwa TAKUKURU

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wakubwa saba wa madini ya Tanzanite mkoani Arusha, wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa tuhuma za kufanya biashara ya madini ya vito kwa njia ya magendo.

Vigogo hao pia wanatuhumiwa kujihusisha na utoroshwaji wa madini kwenda nje ya nchi na ukwepaji wa kodi, kinyume cha sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa na serikali katika biashara hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, katika mkutano na waandishi wa habari jijini hapa jana, aliwataja wafanyabishara hao kuwa ni pamoja na Joel Mollel, maarufu 'Saitoti', meneja wa kampuni ya Gem and Rock Venture ya jijini Arusha na mke wake Caren Mollel ambaye ni Mtanzania mwenye asili ya Asia, Rakesh Kumar Gokhroo anayemiliki kampuni ya kuuza na kununuwa madini ya Colour Clarity jijini.

Wengine ni Daud Saimalie Lairumbe, wakili wa kampuni ya Gem and Rock Venture kutoka Kampuni ya Uwakili ya Northen Law Chambers Advocates & Legal Cunsultants ya jijini Arusha, George Poul Kivuyo, maarufu kwa Lekoo, mchimbaji na mfanyabiashara wa madini na mshiriki wa kibiashara wa Saitoti.

Naiman Mollel, mchimbaji wa madini ya Tanzanite katika mgodi ulioko Mirerani unaomilikiwa na Kampuni ya Gems & Rock Venture ya jijini Arusha pamoja na Ezekiel Laizer, mchimbaji na mfanyabiashara wa madini na mshirika wa kibiashara wa Saitoti wa jijini Arusha.

Mkurugenzi huyo alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa wafanyabiashara Saitoti na Gokhroo kwa kushirikiana na wenzao hao watano wanatuhumiwa kufanya uchimbaji, ununuzi na usafirishaji haramu wa madini ya Tanzanite kutoka katika migodi ya madini hayo yaliyoko Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara bila ya kufuata sheria, kanuni na taratibu. Alisema kuwa tuhuma zilizochunguzwa na zinazoendelea kuchunguzwa ni pamoja na watuhumiwa wote kutumia rushwa kuwashawishi baadhi ya watendaji wa serikali kufanikisha azma yao ya kupunguza thamani ya madini husika, hivyo kuikosesha serikali mapato kwa madini husika kupewa thamani ndogo.

Alisema wafanyabiashara hao wamekuwa wakipata madini bila kufuata sheria, kanuni na taratibu na kuyauza nje ya nchi kinyume cha taratibu, hivyo kuendelea kuikosesha serikali mapato stahiki.

"Pia wamekuwa wakikwepa kulipa kodi halali ya serikali, wamewawezesha wafanyabiashara hao na wabia wao kutumia fedha hizo na kujijengea ukwasi mkubwa uliowawezesha kununua majengo ya kifahari na magari ya kifahari na kuanzisha biashara mbalimbali jijini Arusha pamoja na maeneo mengine nchini," alisema.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema ukwasi huo ambao uchunguzi unaendelea kuubaini unakadiriwa kufikia Sh. bilioni 7.2.

Alisema TAKUKURU imebaini mali kadhaa zinazomilikiwa na watuhumiwa ambazo taasisi hiyo inaendelea kuzifanyia uchunguzi kwa kuwa Saitoti ana mali na biashara katika maeneo mbalimbali jijini Arusha yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.7 huku mke wake akimiliki nyumba na magari yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 610.

Alisema Saitoti na mke wake Caren pia wanamiliki Kampuni ya Azo Africa ambayo inamiliki mgodi, magari na mali nyingine zenye thamani ya Sh. milioni 177.5 na kwa ujumla Saitoti anamiliki mali zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.5. Alisema mtuhumiwa Naiman Mollel anamiliki nyumba na magari yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 574, mfanyabiashara Gohkroo anamiliki magari, fedha taslimu pamoja na madini yenye thamani ya Sh. milioni 895 na mfanyabiashara Lekoo anatuhumiwa kumiliki nyumba na magari yenye thamani ya Sh. milioni 227.

Alisema watuhumiwa wote wanachunguzwa na tayari uchunguzi wake unaendelea vizuri na TAKUKURU kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali na watapelekwa katika vyombo vya sheria.

Alisema endapo wakitiwa hatiani, adhabu stahiki zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na utaifishwaji wa mali zao zilizotokana na ufanyaji wa biashara za madini ya vito kwa njia zilizo kinyume cha sheria.

Brigedia Jenerali Mbungo aliwataka wafanyabiashara wa madini ya vito nchini kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kwa kuwa serikali iko macho na haitakuwa na simile au huruma kwa yeyote atayekiuka.




Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 25-09-2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe **27/09/2020** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRATION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa. Kutoka **INYONGA** kuelekea **KABANGA** kupitia **TABORA** Magari hayo yenye namba za usajili namba za usajili:
   1. **T550 BES/T474BCJ**
   2. **T389 BES/T668 BCJ**
2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **16.0** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.7** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.9** |

3. Njia itakayotumika: **INYONGA hadi KABANGA kupitia MPANDA** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115916602

# Kampeni ya choo yafyeka magonjwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema usimamizi wa usafi wa mazingira na upatikanaji wa maji, umesaidia kupunguza magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Sambamba na hilo, imetaja mikoa inayoongoza kwa kuwa na vyoo bora kuwa ni pamoja na Kilimanjaro, Iringa, Njombe na Dar es Salaam huku Mkoa wa Kigoma, Simiyu, Mara, Songwe na Lindi ikiongoza kwa kutokuwa na vyoo bora.

Akijibu jana maswali ya waandishi wa habari kuhusu udhibiti wa magonjwa hayo, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi, Afya na Mazingira, Anyitike Mwakitalima, alisema hatua hiyo imesaidia kutokuwapo kwa kisa cha mgonjwa yeyote wa kipindupindu kuanzia Julai, mwaka jana hadi sasa.

Pia alisema hali ya upatikanaji wa maji maeneo ya vijijini na mjini umeongeza ambapo kwa mijini hadi kufikia disemba mwaka jana ni asilimia 85 huku vijijini ni asilimia 70.1.

Mwakitalima ambaye pia ni Mkuu wa Sehemu Ndogo ya Maji, Chakula na Usafi wa Mazingira, alisema katika kutekeleza mazingira wezeshi ya kiutendaji, serikali imepanga kuhakikisha angalau kila mkoa unapata gari moja na kila Ofisa afya aliye ngazi ya kata anakuwa na pikipiki.

Awali, akizungumzia maadhimisho ya Siku ya Afya ya Mazingira Duniani inayofanyika leo, Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alisema wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa kampeni ya taifa ya usafi wa mazingira.

Alibainisha kuwa kampeni hiyo inahamasisha jamii kujenga na kutumia vyoo bora na kutumia huduma za kijamii hasa vituo vya kutolea huduma za afya na katika shule.

"Kuna kampeni yenye kaulimbiu: 'Usichukulie Poa Nyumba ni Choo' ambayo inahamasisha ujenzi na matumizi ya vyoo bora na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni,"alisema.

Alieleza kuwa Kampeni hiyo ilikuwa na awamu mbili ambapo kuanzia mwaka 2012 hadi 2016 imesaidia kupunguza kaya zisizokuwa na vyoo kutoka asilimia 6.1 mwaka 2015/16 hadi asilimia 2 mwaka 2019/20.

"Kampeni imesaidia kuongeza vyoo bora kutoka asilimia 40 hadi 63.7 sambamba na kaya zenye vifaa maalumu vya kunawa mikono kuongezeka kutoka asilimia 12.4 hadi 37.6,"alisema.

# Makandarasi kuungana miradi mikubwa

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Makandarasi Wazalendo Tanzania (ACCT), kimetaja sababu zinazowafanya makandarasi wazawa kutokukua ikiwamo kutoshirikishwa kwenye miradi mikubwa.

Kutokana na changamoto hiyo kupitia mkutano mkuu wa tisa wa mwaka wa chama hicho uliofanyika jana jijini Dar Salaam, makandarasi wameona iko haja ya kuungana badala ya kila mmoja kufanya kazi kivyake.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa ACCT, Mhandisi Milton Nyerere, alisema kuungana kwao kutasaidia kuwa na mkakati wa pamoja ikiwamo kuanzisha benki yao kwa sababu zilizopo hazielewi vizuri sekta ya ujenzi.

Mhandisi Nyerere alisema makandarasi wazawa wako tayari kushirikiana na serikali kutekeleza miradi mbalimbali inayoendelea kwa sababu ukuaji wao unategemea fursa za kazi, mitaji na matumizi ya teknolojia kwenye ujenzi.

"Kumekuwa na miradi mikubwa inayotekelezwa ambayo ni fursa katika kukuza uwezo wa makandarasi wazawa. Changamoto ni namna gani wameshirikishwa kwenye miradi hii, hii imebaki kuwa changamoto kubwa," alisema.

Mhandisi Nyerere alisema iko dhana iliyoibuka miaka ya karibuni ambayo imelenga kuonyesha makandarasi wazawa wana gharama za juu wakati wakiomba zabuni.

"Ukweli ni kwamba serikali au mnunuzi yeyote halazimiki kutoa kandarasi kwa yeyote ambaye atajiridhisha kuwa gharama iko nje ya bajeti iliyopangwa," alisema.

Nyerere alisema mikataba ya ujenzi ikizingatiwa malalamiko yote yanayohusiana na utendaji wa makandarasi na gharama za ujenzi hayatakuwapo.

Alisema mikataba ya ujenzi pekee ndiyo silaha inayolinda makandarasi na ununuzi na hutoa suluhisho kwa matatizo ya aina yoyote.

"Tunatoa wito kwa taasisi za serikali kuwa wabunifu wanapopata maagizo ya wanasiasa ya kutumia kampuni za serikali kufanya kazi za umma, inapotokea taasisi inapewa kazi wanashindwaje kuzitoa kwa makandarasi wadogo ili kupunguza mzigo wa usimamizi na kuzingatia bei zilizopangwa," alisema.

Pia alisema kutolipwa kwa wakati miradi mbalimbali ambayo makandarasi wameifanya, imewarudisha nyuma wengi kukua kiuchumi na kujikuta katika madeni au kufilisiwa.

"Ikumbukwe mkandarasi anapoomba malipo ya kazi anayoifanya kwa taasisi ya serikali anatakiwa kuambatanisha malipo ya kabla hivyo kumpa jukumu la kulipa kodi kabla hajalipwa malipo na wakati mwingine huchelewa mpaka miaka mitano na kujikuta wanatoa kodi katika malipo ambayo siyo ya kazi," alisema.

Pia aliiomba serikali iweke nia ya dhati ya kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zinazolenga kuwainua kiuwezo makandarasi wazawa kwa wale wa kigeni kutoa kazi kwao.

Katika mkutano huo makandarasi hao walijadili kuhusu namna ambavyo wataweza kuungana na kuwa wamoja ili waweze kushiriki kikamilifu shughuli za kujenga uchumi wa nchi.

Kuhusu changamoto ya malipo kabla iliyotolewa na ACCT, Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Godwill Wanga, aliahidi wataiangalia na Waziri wa Fedha na Mipango ili kuona uwezekano wa kuiondoa.

Wanga aliahidi changamoto zote zilizobainishwa na baraza hilo ataziwasilishwa eneo husika ili kuona namna ya kuzitatua.

"Nina wapongeza kwa kazi kubwa ya kuanzisha kituo cha mafunzo kwa mafundi mkoani Arusha zenye gharama ya Sh. Milioni 150 ambacho kwa mwaka huchukua awamu tatu mpaka nne kupiga msasa mafundi wapatao 72 katika fani za ujenzi," alisema.



Lori la mizigo aina ya Fuso likiwa limekwama kwenye matope katika eneo korofi la Timba, Kijiji cha Bombani, wilayani Muheza, Mkoa wa Tanga juzi. Wananchi wameomba serikali kukarabati eneo hilo, kwani limekuwa kero kubwa kwa muda mrefu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# DC aagiza tathmini ya fedha za halmashauri

**Na Godfrey Mushi, HAI**

SERIKALI imeagiza Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kufanya upya tathmini ya mgawo wa fedha kwa vikundi vyote vilivyopatiwa mikopo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa makundi maalum ya jamii.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, aliagiza hayo jana baada ya kukabidhi Sh. milioni 30.1 kwa vikundi vya wajasiriamali.

"Ofisa Maendeleo ya Jamii, ninataka uniletee taarifa ya tathmini kuhusu utekelezaji wa mpango wa serikali kuhusu utoaji wa mikopo ya wanawake, vijana na walemavu. Nia ya serikali ni kuwainua wananchi wake kiuchumi na kuleta maendeleo kwenye jamii.

"Kwa hiyo, tunapaswa kujiridhisha tena kama mpango huu umefikia malengo yake vyema. Lakini pia ninasisitiza tena, ondokeni ofisini, nendeni mkawape ushauri wa namna ya kuimarisha biashara zao," aliagiza.

Kabla ya makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alisema halmashauri yake itaendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kutokana na asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani.

Baada ya hafla hiyo, mmoja wa wanakikundi cha Ebeneza kilichoko Machame kinachojihusisha na kilimo cha mboga, Naomi Changari, aliishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu wa utoaji wa mikopo, akisema fedha hizo zimekuwa chachu ya maendeleo kwa wajasiriamali katika wilaya hiyo. Katibu wa Kikundi cha Tauwa kilichoko Kambi ya Raha, Shabani Omary, alisema wamefurahi kupata kile walichokuwa wanakisubiri, huku wakiishukuru serikali kwa kutambua matatizo yanayowakabili vijana.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya Hai, imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. 179,602,904 (milioni 179.6) kwa vikundi vya wajasiriamali vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

# Mgombea aahidi kuanzisha hifadhi ya wanyamapori

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Malinyi, kupitia NCCR-Mageuzi, Kennedy Chaya, amesema ikiwa wananchi watamchagua, atahakikisha inaanzishwa Hifadhi ya Wanyamapori ya Malinyi.

Akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya kampeni, Chaya alisema katika wilaya ya Malinyi kuna mbuga kubwa na ndani yake kuna wanyama wa kila namna katika mbuga hiyo, ambayo kwa sasa serikali inaitambua kama pori tengefu.

"Nikiwa mbunge nitaishauri serikali kuona umuhimu wa kuanzisha hifadhi ya Malinyi kwenye hilo pori tengefu, ambalo limepita kila kata wilayani Malinyi," alisema.

Chaya alisema wilaya hiyo itakapokuwa na hifadhi kutakuwa na faida kubwa kwa kupata fedha za kigeni na kwamba mapato ya ndani yataongezeka na ajira zitakuwa nyingi kwa vijana.

"Wananchi tukiwa na hifadhi ya Malinyi unakuwa mji wa kitalii fedhaa zinakuwa nyingi kutajengwa hoteli maendeleo yataonekana na kama mnavyofahamu shughuli za kitalii zina fedha nyingi, malinyi tutakuwa tunapokea wageni mara kwa mara. Sasa katika mazingira kama haya, kwa nini barabara za lami kama ya Malinyi-Ifakara ambayo ni kero kubwa kwetu na ile ya Lupilo, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo, Londo Kitanda hadi Namtumbo (barabara ya Songea) sizijengwe," alisema.

Kuhusu elimu, alisema pamoja na serikali kutoa elimu bure kutoka shule za msingi hadi sekondari, ziko changamoto nyingi katika jimbo hilo ikiwamo uhaba wa walimu, vyumba vya madarasa na vifaa vya kufundishia hali ambayo inasababisha kushuka kwa kiwango cha ufaulu.

"Mkinichagua nitasimamia uanzishaji elimu kazi Malinyi hasa kwa wale wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, lakini hawajabahatika kufaulu kuendelea na masomo ya sekondari sambamba na wale wanaofeli kidato cha nne," alisema.

Aidha, aliahidi kuanzisha benki za wananchi ambazo zitasaidia wakulima wadogo, wavuvi na wafugaji kuweza kukopeshwa mikopo yenye masharti nafuu.




Wananchi wa Jimbo la Kwimba, wakimsikiliza Mjumbe wa Kamati Kuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani), wakati akiwahutubia katika mkutano wa kampeni, uliyofanyika katika viwanja vya sokoni, juzi. **PICHA: OWM**

# Majaliwa asema CCM inastahili kuendelea na mipango imara

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania wachague chama hicho, ili kiendelee kuwaletea maendeleo.

Majaliwa alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Sumve, Kwimba mkoani Mwanza, kwenye mkutano uliofanyika kwenye viwanja vya Misheni.

"Chagueni CCM, chama chenye mipango ya maendeleo na ya kueleweka. Chama chenye mipango ndani ya kitabu chenye kurasa 303. Naomba kura zenu, ili tuwaletee maendeleo," alisema na kuongeza kuwa:

"Zamani tulikuwa na kitabu kidogo cha kurasa 236, lakini sasa hivi tuna buku kubwa zaidi. Tukitekeleza yote haya, mambo si yatakuwa mazuri zaidi?"

Majaliwa ambaye yuko mkoani Mwanza, kumuombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, alitumia fursa hiyo kumwombea kura mgombea ubunge wa jimbo la Sumve, Kasalali Mageni, mgombea udiwani wa kata ya Sumve, Gervas Kitwala, na wagombea udiwani wengine wa kata zote za Wilaya ya Kwimba.

"Ninaomba kura kwa wapenzi wa vyama vyote, pigeni kura nyingi sana kwa Magufuli, mgombea ubunge Kasalali na madiwani wote, ili mpate wawakilishi wengi zaidi kupitia viti maalum," alisema.

Akielezea mafanikio kwenye sekta ya maji wilayani humo, Majaliwa alisema Sh. bilioni mbili zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya Igumangobo, Igunguhya na Nyanhiga, upanuzi wa mradi wa maji Kadashi-Nyashana, upanuzi wa mradi wa maji Hungumalwa na upanuzi wa mradi wa maji KASHWASA kwenda kijiji cha Jojiro.

Fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi mingine ya maji, alisema ni Sh. milioni 118.6 kwa ajili ya miradi ya uchimbaji wa visima vya Nkalalo na Lyoma na uchimbaji wa kisima katika mji wa Sumve.

Kuhusu barabara, Majaliwa alisema serikali iliunda Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), ili ifuatilie na kukagua maeneo korofi na watoe makadirio ya matengenezo, ili zitafutwe fedha za ujenzi.

"Malengo ya Serikali ya kuboresha njia za usafirishaji ni pamoja na kuimarisha barabara zote zinazounganisha kijiji na kijiji, kata na kata, wilaya na wilaya ikiwa ni pamoja na madaraja yanayopita kwenye barabara hizo kwa kuyaingiza kwenye mpango, ili njia hizo ziweze kupitika," alisema.

## Wagombea waonywa kutoheshimu matokeo

**Na Innocent Ng'oko, MWANZA**

UMOJA wa Wapigakura Tanzania (UWAKUTA), umewatahadharisha wagombea wa urais, ubunge na udiwani kutoka vyama vyote vya siasa kuwa ni lazima watii na kuheshimu uamuzi wa wapigakura katika matokeo ya uchaguzi.

Akizungumza na gazeti hili ofisini kwake jana, Mratibu wa UWAKUTA, Peter Mpeleka, alisema jana kuwa, kumekuwa na tabia ya baadhi ya wagombea wa udiwani, ubunge na urais kuingilia uamuzi wa wapigakura kwa kubeza matokeo.

Mpaka sasa, alisema umoja huo umeshatembelea maeneo mbalimbali ya nchi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wapigakura kuhusu umuhimu wa kushiriki kwa wingi, kuwachagua wagombea wa nafasi mbalimbali wanaowataka kwa ajili ya maendeleo yao.

Mpeleka alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wanasiasa kulalamikia matokeo bila sababu za msingi, hivyo kusababisha taharuki kwa wapigakura na wananchi kwa ajili ya mstakabali wa amani ya nchi yao.

Alisema umoja huo unashirikiana na vyombo vya dola, kuhakikisha wanawatia nguvuni baadhi ya watu, ambao wamekuwa na tabia ya kuwahadaa wapigakura kwa kununua shahada zao za kupigia kura katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu wa nchi.

Mpekeka pia, alivitaka vyombo vya dola kulinda usalama wa wapigakura kwa lengo la kuhakikisha wanakwenda katika vituo vya kupigia kura na kutimiza wajibu wao wa kuwachagua viongozi wanaowataka, bila ya bugudha yoyote. Alisema, vyombo vya dola visije vikajiingiza katika kuwanyanyasa wapigakura kwa namna yoyote ile na kuwa jukumu lao ni kuhakikisha wanalinda usalama wa wapiga kura katika maeneo ya vituo vya kupigia kura.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msimu huu Ligi Daraja la Kwanza imulikwe zaidi

**KIPENGA** cha kuanza kwa Ligi Daraja la Kwanza msimu huu wa 2020/21, kimepulizwa rasmi baada ya mapema wiki hii Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kutangaza ratiba ya ligi hiyo ambayo msimu ujao wa 2021/22, zitashuhudiwa tena timu mbili zikipanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Bara.

Msimu uliomalizika tulishuhudia timu tatu, Gwambina FC na Dodoma Jiji FC zikipanda Ligi Kuu moja kwa moja, wakati Ihefu FC ikipanda kupitia mechi ya mchujo baada ya kuitoa Mbao FC ya Ligi Kuu.

Katika ligi hiyo ambayo TPLB imetangaza itaanza rasmi kutimua vumbi Oktoba 9, mwaka huu, itashirikisha timu 20 zilizogawanywa makundi mawili, A na B kila moja likiwa na timu 10, na kinara wa kila kundi atapanda Ligi Kuu moja kwa moja, wakati timu zitakazoshika nafasi ya pili kwenye kila kundi zitacheza mechi za mchujo na timu kutoka Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Kundi A linaundwa na African Lyon, African Sports, Boma FC, Gipco FC, Lipuli, Majimaji FC, Mawenzi Market, Mbeya Kwanza FC, Ndanda FC na Njombe Mji, wakati Kundi B likiwa na Alliance FC, Arusha FC, Fountain Gate FC, Geita Gold FC, Kitayosce FC, Mbao FC, Pamba FC, Rhino Rangers FC, Singida United na Transit Camp FC. Kwa ujumla ni ligi ambayo, itakuwa na ushindani mkubwa hasa kutokana na kujumuisha timu nne zilizoshiriki Ligi Kuu, msimu uliomalizika wa 2019/20; Lipuli FC, Mbao FC, Ndanda FC na Singida United, lakini pia zikiwamo timu zilizoonyesha ushindani mkubwa Ligi Daraja la Kwanza msimu huo wa 2019/20.

Kama ambavyo ushindani umeongezeka katika Ligi Kuu msimu huu, tunaamini ndivyo itakavyokuwa Ligi Daraja la Kwanza na hata Daraja la Pili, baada ya Septemba 10, mwaka huu Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutangaza kuingia mkataba wa udhamini wa miaka miwili na Kampuni ya Paymaster wenye thamani ya Sh. milioni 240 kwa ajili ya kuidhamini ligi hizo. Kwa kipindi kirefu hadhi, heshima na hata ushindani kwenye Ligi Daraja la Kwanza na la Pili ulipungua kutokana na timu nyingi shiriki kukabiliwa na ukata, hivyo kushindwa kutoa upinzani mkubwa katika michezo yao, hasa kwa kuwa zilizo nyingi hazina wadhamini wao binafsi.

Pamoja na kwamba fungu zitakalolipata kutoka kwa mdhamini huyo wa TFF, haliwezi kutosheleza mahitaji ya timu kwa msimu mzima, tunaamini litapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto kama za usafiri, malazi na hata posho kwa wachezaji, ili kujituma zaidi. Kutokana na matarajio ya kuwapo ushindani mkubwa msimu huu katika ligi hiyo, tunaitaka TFF na TPLB kuelekeza umakini zaidi katika mechi zote, kama ambavyo imeongeza umakini kwenye Ligi Kuu kwa kuonyesha mechi zote msimu huu na kuzidi kufunga viwanja vibovu. Ingawa Ligi Daraja la Kwanza haionyeshwi mubashara kupitia luninga, lakini tunataka kuona umakini ukiongezwa katika vituo vyote, ikiwa ni pamoja na TPLB kutovifumbia macho viwanja vibovu, kama ambavyo imekuwa ikivishughulikia kwa kuvifungia vile visivyokidhi viwango vinavyotumiwa na timu za Ligi Kuu Bara.


Lengo letu ni kutaka kuona ushindani wa kweli na timu zinazopanda Ligi Kuu msimu ujao, zikiwa ni zile zenye sifa stahiki na zilizoonyesha kiwango kwa kushinda mechi zake kihalali, bila kubebwa kwa aina yoyote ile. Tunasema hivyo kutokana na kero nyingi na changamoto, ambazo zimekuwa zikijitokeza katika ligi hiyo, mara nyingi kufumbiwa macho kwa kutoshughulikiwa ipasavyo, hatua ambayo baadhi ya timu zinazopanda daraja hushindwa kutoa upinzani mkubwa Ligi Kuu, jambo linalotia walakini katika mchakato wao wa kusaka nafasi hiyo. Kwa mujibu wa mfumo mpya wa Ligi Kuu uliotangazwa na TPLB, msimu ujao wa 2021/22, Ligi Kuu Bara itashirikisha timu 16, hivyo tunataka kuona timu zitakazopanda kutoka Ligi Daraja la Kwanza, zikiwa zile zilizoonyesha ubora na kushinda kihalali bila kubebwa kwa namna yoyote ile ili kuja kuongeza ushindani.

Tunaamini kama hayo yatatekelezwa, msimu ujao utashuhudia ligi ngumu zaidi, ambayo itazidi kuwa kivutio kwa wachezaji kutoka nje kuja kucheza nchini, lakini pia ikiwavutia wawekezaji wengi kutoka nje na ndani ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Maneno makali hayavunji mfupa

**MANENO** tu hayawezi kuvunja mifupa, hata yakawa makali jinsi gani. Methali hii hutumiwa na mtu anayepuuza maneno yaliyosemwa na mtu mwingine na ambayo hayawezi kumdhuru kwa namna yoyote au hayamzuii kutekeleza jambo alitakalo. Watu wengine huamini kwamba, maneno ya kuudhi huweza kumtia uchungu mkali binadamu.

Aidha, maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hayarudi. Maana yake neno analotamka mtu ni kama mkuki, likitoka halirudi na huweza kuleta madhara. Methali hii yatusihi tuwe na tabia ya kuyatafakari maneno tuyasemayo kabla. Ni vizuri kulipima neno, kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye.

Mashabiki ni watu wenye mapenzi na hamasa kubwa ya jambo au kitu. Mara nyingi mashabiki wa kandanda, hasa kwa timu wazipendazo ni wepesi wa kusema maneno ya maudhi na hata kuwatukana wapinzani wao hadharani, bila kujali tofauti zao kiumri. Idadi kubwa ya watu wa tabia hii si wanachama wa klabu husika, ila hufuata mkondo baada ya ushindi wa timu za kandanda, hasa Simba au Yanga inapoishinda ingine. Hawana wajualo kuhusu uendeshaji wa klabu zao, wala usajili wa wachezaji na makocha wao.

Wahenga walisema "Mdomo siri ya gunda (baragumu)." Maana yake siri yoyote aliyo nayo binadamu hujulikana na gunda kwa vile mdomo na gunda huhusiana sana. Mtu anayeweza kuzijua siri za mwengine ni yule anayehusiana naye kwa karibu. Mathalani, siri za mume azijua mkewe, kama mume anavyozijua siri za mkewe.

Husemwa na kuandikwa kwenye vyombo vya habari za michezo kuwa, Simba na Yanga ni 'watani wa jadi.' Sikubaliani na hilo kwani timu hizo, nionavyo, zastahili kuitwa 'wapinzani wa jadi' kwa jinsi zilivyo na uhasama kama walivyo Waarabu na Wayahudi! Kisa ni gozi la ng'ombe. Ebo! (tamko linaloonesha hisia ya dharau inayotokana na kukasirika au kutoridhika). Ndivyo zinavyohasimiana Simba na Yanga ingawa zamani zilikuwa moja.

Ni wanachama wachache wanaofungua vinywa vyao na kutoa maneno ya matusi wakati timu zao zinaposhinda, lakini wengi wao ni mashabiki wasiojua 'be' wala 'te' kuhusu klabu zao. Waungwana hawaonekani mitaani wakiropoka na kuwatukana wenzao matusi ya nguoni! Kama timu mojawapo katika hizo ikitoa sare kwa timu ingine na kushangiliwa kuna ubaya gani hata mama zao watukanwe hadharani?

Msimu uliopita wakati Simba ilipotangulia kuifunga Yanga mabao 2-0, lakini ikasawazisha na kuwa sare ya mabao 2-2 mpaka mchezo ulipomalizika, wanachama na mashabiki wa Yanga walifurahi sana. Siku iliyofuata nikiwa maeneo ya Kariakoo barabara ya Sikukuu, nilimsikia shabiki wa Simba akisema: "Hiyo sare Yanga wanachonga sana kwani kwao ni ushindi ..." kisha akatukana tusi la nguoni, ambalo hata yeye alipitia njia hiyo hiyo kuiona dunia!

Naishi eneo la Kipunguni 'A' kupitia Banana, kuelekea maeneo ya Kitunda na kwingineko. Pale Banana nafahamika na wauza matunda na mboga za aina mbalimbali; hata kwenye kituo cha daladala na bodaboda huniita kwa jina langu la mchezo wa maigizo (Mambo hayo) yaani 'Baba Bishanga' au 'Mzee Kambaulaya.' Wote hao wanajua uanachama na mapenzi yangu kwa Yanga; hivyo timu yangu inaposhindwa hunipa pole na wengine hunitania kwa maneno ya kawaida. Mimi huwafuata wapinzani wangu (Simba) walio waungwana na kuwapongeza kwa ushindi nao hunipongeza Yanga, inapoishinda timu yao. Huo ndio uungwana, yaani hali ya mtu kuwa tayari kumfanyia mwingine wema na insafu (moyo wa ushirikiano).

Sikatai kutaniwa na watani wangu (Simba) timu yangu inaposhindwa. Huwapa nafasi ya kusema watakavyo, bila matusi na wanapomaliza tambo zao, huwaaga kwa kuwapongeza huku nikijitapa kuwa Yanga ndo kiboko kwao, kwani imetwaa Kombe la Ligi Kuu mara nyingi zaidi kuliko timu yoyote nchini ikiwemo Simba yao.

Kwa kuwa Watanzania twaitana ndugu, ni vema nitumie methali ya wahenga wetu waliosema: "Kuishi na ndugu ni kuvumiliana." Kwamba mtu anayeishi na ndugu yake lazima amvumilie. Twafunzwa tuwe na subira na watu wanaotuhusu kama vile jamaa wa karibu. Pia "Kuishi kwingi ni kuona mengi." Angalau Mungu ameniwezesha kufikisha umri wa miaka 82 tangu nilipozaliwa tarehe 24/8/1938. Mtu anayeishi kwa muda mrefu huwa ameshuhudia mengi. Methali hii yatunasihi kutowadharau wazee kwa kuwa wana busara inayotokana na uzoefu wa miaka mingi maishani. Alhamdulillahi! (Tamko la kuonesha shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa mema anayoendelea kunifanyia.)

# Waziri achukua uamuzi mgumu makandarasi miradi umeme REA

**Na Mwandishi Wetu,**
TABORA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametangaza uamuzi mgumu kwa makandarasi wa umeme na kwamba kuanzia sasa ni marufuku kwa makandarasi watakaotekeleza miradi ya usambazaji wa umeme vijijini, kupewa kazi katika mkoa zaidi ya mmoja.

Pamoja na uamuzi huo, amesema kuanzia sasa makandarasi hao watapewa kazi kwa kila wilaya bila kujali idadi ya vijiji vilivyopo.

Dk. Kalemani alisema hayo kwa nyakati tofauti mkoani Tabora alipokuwa akizindua mradi wa usambazaji wa umeme katika kila kitongoji nchini uliofanyika katika wilaya za Uyui na Nzega juzi.

Alisema mradi huo utavifikia vitongoji vyote nchini bila kujali kuwa vimefikiwa na umeme au la huku akibainisha kuwa lengo la kuwapatia makandarasi hao kazi za wilaya ni kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa haraka ndani ya muda mfupi na kwa wakati.

"Kuanzia sasa makandarasi wote wanaotekeleza miradi ya REA (Wakala wa Nishati vijijini) nchini, watakuwa wanapewa kazi za kutekeleza miradi hiyo kwa kila wilaya bila kujali idadi ya vijiji vilivyopo. Mkandarasi anaweza pewa wilaya moja yenye vijiji 20 au 70 jukumu kubwa likiwa ni kumaliza kazi kwa wakati. Hii itaondoa changamoto (tatizo) ya (la) kutomaliza miradi kwa wakati au wengine walikuwa wanaelekeza nguvu nyingi katika eneo A na kuacha eneo B, ama kufanya maeneo yote kwa kusuasua," alisema Dk. Kalemani.

Alisema utaratibu huo utawezesha ukamilishaji wa miradi ya namna hiyo kwa wakati na kwamba mkandarasi yeyote atakayechelewesha mradi, atachukuliwa hatua za kimkataba, kisheria na za kuisimamizi kwa kuwa maeneo ya utekelezaji wa miradi imepunguzwa tofauti na awali.

Sambamba na hilo, alisema hakutakuwa na muda wa nyongeza kwa yeyote atayechelewesha mradi na badala yake atakatwa asilimia 10 ya fedha zake kama adhabu na mradi huo atapewa mtu mwingine.

"Hatua hii itaondoa visingizio na sababu za baadhi ya makandarasi wenye tabia hiyo kwa lengo la kuchelewesha mradi, kwa sababu wengine walikuwa wanasingizia ukubwa wa eneo, wengine miundombinu au vifaa havitoshi ana kufika kwa wakati, sasa hii itamaliza sababu zote za kuchelewesha miradi," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Dk. Kalemani alilisisitiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwakatia umeme wateja wenye madeni sugu ili kupata fedha za kulijengea uwezo shirika kutoa huduma bora na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Aliwaagiza mameneja wa kanda, mikoa na wilaya kutowaonea huruma wateja wa namna hiyo kwa kuwa wanarudisha nyuma maendeleo ya shirika na kusababisha wananchi wengine kukosa huduma bora kwa wakati.

## Wizara yahamasisha elimu watu wazima

**Na Romana Mallya**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa James Mdoe, amesema juhudi za pamoja zinahitajika katika ngazi zote ili kupunguza au kuondoa tatizo la vijana na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Profesa Mdoe alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua Mpango Mkakati wa Kitaifa wa miaka mitano kuanzia 20/21 hadi 24/25 wa kukuza na kuendeleza kisomo na elimu kwa umma.

Alisema kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, idadi ya vijana na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu ni asilimia 22.

"Hii ni idadi kubwa hivyo jitihada za ziada zinatakiwa kuondoa hali hii, ninaamini mkakati huu utapunguza idadi hii kwa kuwajengea uwezo wa kuyatambua, kuyatafsiri na kuchukua hatua sahihi za kukabiliana na changamoto zilizoko katika mazingira yao kwa kutumia stadi za KKK," alisema.

Profesa Mdoe alitoa rai kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ambao ndiyo waratibu wakuu wa mpango huo, kuusimamia vyema ili watekelezaji wakiwamo Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wadau wengine wautekeleze kama ilivyopangwa ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Pia, aliwataka wadau wote wa elimu ya watu wazima kuutumia mpango mkakati huo katika kuanzisha na kuyaendeleza madarasa ya kisomo katika maeneo yao.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Michael Ng'umbi, alisema utekelezaji wa miradi na programu hizo umewasaidia vijana na watu wazima walionufaika, kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Alisema taasisi ina utaratibu wa wanachuo wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo, kuanzisha na kuwezesha madarasa ya kisomo sehemu mbalimbali kwa kipindi chote wanapokuwa mafunzoni.

Kuhusu mkakati uliozinduliwa jana, alisema unalenga kubuni na kuendeleza mipango ya elimu bora na yenye manufaa kwa watu wazima na umma kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Tamaduni (UNESCO), Tirso Dos Santos, alisema ili kutimiza lengo la kujua kusoma na kuandika ulimwenguni, juhudi bora zaidi na njia mpya ya kisiasa ni muhimu katika ngazi zote kitaifa na kimataifa.

Dos Santos pia alitaka wadau wote wa elimu kuendelea kudumisha na kujitolea kukuza elimu ya kitaifa na kimataifa.



Mwenyekiti Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Peter Mwambuja (wa pili kushoto) akikabidhi cheti cha kuwatambua wanafunzi waliofanya vizuri zaidi kwenye mitihani ya kidato cha sita mwaka 2020 katika masomo ya biashara, kwa mwanafunzi wa shule ya Shabani Robert, Saadia Yussuph, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Maingu Mwigamba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bei wanyama mbegu karibu na bure

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WIZARA ya Maliasili na Utalii imepunguza bei za wanyama wa mbegu kwa asilimia 90 ili kuwawezesha wananchi kumudu gharama za ufugaji wanyamapori katika mashamba, ranchi na bustani za wanyamapori.

Lengo la hatua hiyo pia ni kuwezesha kuwa na uhakika wa kupatikana nyamapori za kuuza kwenye bucha zitakayofunguliwa hivi karibuni Tanzania Bara.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye warsha ya kutangaza maeneo rasmi ya kuanzisha bucha za nyamapori iliyofanyika makao makuu ya ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), mjini hapa.

Alisema kupunguzwa kwa gharama hizo kutasaidia wananchi kumudu gharama za ufugaji kwa kuwa ufugaji wa wanyamapori ndio chanzo kikuu cha nyama itakayouzwa kwenye bucha.

"Kwa mfano bei ya wanyamapori kama nyati imepungua kutoka Sh. milioni 4.1 hadi Sh. 210,000, swala pala kutoka Sh. 300,000 hadi Sh. 90,000" alisema Nzuki.

Alisema vyanzo vingine vya upatikanaji wa nyamapori ni pamoja na uwindaji wa kitalii na uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na kwamba uwindaji wa kitalii mara nyingi huchukua vitu mbalimbali na nyama zikabaki ambazo zitafikishwa kwa wananchi kupitia bucha zinazoanzishwa.

Dk. Nzuki alisema mikoa 23 kati ya 26 Tanzania Bara itanza kutoa huduma za bucha za nyamapori na mikoa ya Songwe, Mara na Rukwa itaongezeka baada ya kukamilika utaratibu wa kiutendaji.

Alisema wizara imeweka vigezo vya magari maalum yatayotumika kama bucha maalum za kubeba na kuuzia nyamapori (mobile butcher) ambayo yatapatiwa leseni za kutoa huduma za usambazaji na uuzaji wa nyama kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mpaka sasa, alisema wamepokea maombi 25 ya Watanzania wanaokusudia kuanzisha bucha za nyamapori ambayo yatapitiwa na kamati maalum ambayo inatarajia kukutana Oktoba 12, mwaka huu, na kutoa leseni za uanzishaji wa bucha hizo.

Naye Naibu Kamishna wa Uhifadhi Huduma za Utalii na Biashara wa TAWA, Imani Nkuwi, alisema mamlaka imewaonya wote wanaofikiria kuanzishwa kwa biashara ya bucha za nyamapori kuwa ndiyo njia ya kufanya ujangili, wasifikirie hivyo bali watambue kuwa TAWA imejipanga kudhibiti na kusimamia suala hilo kisheria.

Alisema suala la uanzishaji bucha za nyamapori lilikuwapo tangu mwishoni mwa miaka ya 1980 chini ya kampuni ambapo lilihamishiwa idara ya wanyamapori Wizarani na kuendelezwa kwa mujibu wa sheria na kanuni na kusitishwa mwaka 1989 baada ya kuwapo kwa ujangili mkubwa.

## Wamiliki shule binafsi kuteta

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa Shule Binafsi Tanzania (TAPIE), kimepanga kufanya mkutano wake mkuu maalum Oktoba, mwaka huu, ambao utawashirikisha wanachama wote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa TAPIE, Prof. Aloyce Maro, mkutano huo utafanyika katika ukumbi wa St. Dominica Nyakahoja, Nyamagana mkoani Mwanza, Oktoba 14, mwaka huu.

"Tunawaalika wanachama wote kuhudhuria mkutano mkuu maalum, wanachama wote mnatakiwa kufika bila kukosa ili pamoja na mambo mengine, tupate taarifa za maendeleo ya chama chetu kwa kipindi cha miaka miwili na kujaza nafasi wazi za uongozi ngazi ya taifa," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema kwenye mkutano huo, wanachama watajadiliana kuhusu changamoto mbalimbali za kiuwekezaji na kiuendeshaji wanazokabiliana nazo na namna ya kuzitatua.

Prof. Maro alisema TAPIE ni asasi isiyo ya kiraia iliyosajiliwa na Msajili wa Asasi za Kiraia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na ni chombo kinachowaunganisha wamiliki wa shule binafsi zilizosajiliwa na zinazotoa huduma kuanzia elimu ya awali hadi sekondari.

Alisema lengo kuu la TAPIE ni kuhamasisha wamiliki kutoa elimu bora kwa kuwahimiza na kuwawezesha wamiliki na wawekezaji katika elimu msingi (awali hadi sekondari) kutoa elimu bora inayozingatia sera, kanuni na miongozo ya serikali.

Alitaja lengo lingine kuwa ni kuwaleta pamoja wawekezaji na wamiliki wa shule binafsi ili kuwa na jukwaa la mijadala na midahalo kuhusu uwekezaji na uendeshaji wa shule nchini kwa maslahi ya jamii nzima.

"Umoja huu pia unatupa nafasi ya kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine wa elimu ili kupata majibu ya changamoto mbalimbali zinazoathiri maendeleo na utoaji wa elimu bora nchini," alisema.

# Mafunzo TBS yadhihirisha mkakati kufukia lengo la Tanzania ya viwanda

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SERIKALI mkoani Tanga imesema mafunzo yanayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa wafanyabiashara kuhusu usajili wa majengo na bidhaa za chakula na vipodozi ni uthibitisho wa azma ya serikali kufanikisha malengo ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Judica Omary, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo yanayoendeshwa na shirika hilo kwa wajasiriamali kuhusiana na usajili wa majengo na bidhaa za chakula na vipodozi.

Alisema uongozi wa mkoa unaamini kuwa mafunzo hayo ni njia mwafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuliletea taifa maendeleo ya haraka kulingana na fursa zilizopo hasa kwenye sekta za viwanda, kilimo, biashara, uvuvi na maeneo mengine mengi.

"Mafunzo haya yamekuja kwa wakati mwafaka ambapo serikali imeazimia kwa dhati kabisa kuendeleza viwanda ili kutoa ajira katika kada mbalimbali pamoja na kuziwezesha bidhaa zetu kushindana katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya Tanzania," alisema Omary.

Alisisitiza kwamba wanaona mwelekeo mzuri chini ya usimamizi wa Rais John Magufuli ambao umewezesha nchi kutoka katika uchumi wa chini na sasa imeingia uchumi wa kati.

"Nchi yetu kuwa na uchumi wa kati imekuwa chachu ya kutufanya tuendelee kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa hiyo tusibweteke. Ni muhimu washiriki wa mafunzo haya msikilize kwa makini na kuchangia mada hizi kwa uwazi ili kupata utaalamu mtakaoutumia kwenye shughuli zenu," alisema.

Alifafanua kwamba ni imani yake kuwa baada ya mafunzo hayo watakuwa wamepata elimu, itakayowawezesha kusajili maeneo ya shughuli zao za biashara.

Aliwataka washiriki kutumia fursa hiyo kujadili kwa pamoja na wataalamu changamoto mbalimbali zinazohusiana na huduma zinazotolewa na TBS zikiwemo taasisi zingine zikiwamo Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Ofisi ya Ofisa Biashara, Afya na Maendeleo ya Jamii.

Kwa upande wa Tanga, Omary alisema TBS inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na watendaji walioko katika kalmashauri ili kurahisisha kufikisha huduma kwa wananchi.

"Kwa hiyo nazielekeza halmashauri zote za mkoa wa Tanga kuendelea kutoa ushirikiano kwa TBS iii kuwahudumia wananchi wetu kwa ufanisi na kwa haraka," aliagiza.

Alitoa mwito kwa shirika hilo kuendelea kuongeza nguvu katika kuboresha uhusiano huu na halmashauri za mkoa huo hasa kwa kushirikiana kwa karibu na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mafunzo hayo yanalenga kutoa uelewa kuhusu taratibu za usajili wa majengo na bidhaa za chakula na vipodozi, madhara ya vipodozi vyenye viambata sumu pamoja na kufanya usajili wa majengo yanayohusiana na shughuli za uzalishaji, utunzaji na uuzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi hususan kwa yale ambayo hayajafanyiwa usajili au muda wa usajili uliofanywa awali ulifikia ukomo.

Kundi lililolengwa kwa ajili ya mafunzo hayo ni wajasiriamali ambao ni sehemu muhimu katika sekta binafsi inayochangia pato la taifa, kuongeza ajira na kuondoa umasikini nchini.




Mafundi ujenzi wakijenga chemba ya maji taka katika ujenzi unaoendelea wa barabara ya Shekilango, eneo la Sinza, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mauaji ya wazee yapungua kwa kasi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa masuala ya wazee nchini, wamekutana kujadili hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kutokomeza mauaji dhidi ya wazee, leo jijini hapa.

Mauaji ya wazee yamepungua kutoka 557 mwaka 2014 hadi 74 mwaka jana huku ikibainishwa kuwa wastani wa vitendo hivyo umeshuka hadi kufikia wazee 10 kwa mwaka, imeelezwa.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Sayi Magessa, alisema hayo wakati wa mkutano wa wadau wa masuala ya wazee unaofanyika jijini hapa.

Akifungua mkutano huo jana kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya - Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, Sayi alisema kupungua kwa mauaji hayo ni matokeo ya mkakati huo.

"Mkakati huu umesaidia sana kupunguza mauaji hayo na hadi sasa idadi inazidi kupungua hadi kufikia mmoja hadi tisa. Kipindi kama hiki cha uchaguzi hali ilikuwa mbaya pia hata kwa walemavu kutokana na imani potofu tu," alisema. Awali, akimkaribisha mgeni rasmi kufungua mkutano huo, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ngóndi, alitoa rai kwa vyombo vinavyohusika na upelelezi pamoja na hukumu kuhusu mauaji ya wazee kusaidia ili jamii itambue kuwa jambo hili ni kosa kwa kuwa wazee wana haki ya kuishi na kufurahia maisha. "Mwisho wa siku tutatoka na maazimio ambayo kwa miaka iliyobaki historia ya kuua wazee iwe tumeisahau katika nchi yetu. Nitoe rai kwa wenzetu wanaoshughulikia mifumo ya jinai kusaidia mchakato wa kupeleleza mauaji ya wazee pamoja na kuwahukumu wote wanaohusika, hii itatoa ujumbe kwa jamii kuwa hii si sahihi," alisema.

Naye Meneja wa Programu Haki kwa Wazee na Ushirikiano wa Wadau kutoka helpage International, Joseph Mbasha, alisema kutokana na ushirikiano na jitihada za wadau, nchi inakwenda vizuri katika kutokomeza mauaji ya wazee. Mbasha alibainisha kuwa takwimu zimepungua pamoja na kuwa barani Afrika nchi nyingi zilikumbwa na janga hilo kutokana na imani potofu.

Mmoja wa wazee walioshiriki mkutano huo, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Mashirika Yanayotetea Wazee nchini, Cotilda Isidory, alisema tangu serikali kupitia vyombo vyake mbalimbali iingilie kati suala la mauaji ya wazee, hivi sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa.



HABARI DODOMA

# Wakuu taasisi za serikali watakiwa kuheshimu sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza wakuu wa taasisi na idara za umma kusimamia ipasavyo Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019 na kanuni zake ili kujiepusha na ukiukwaji wowote ambao adhabu yake ni kifungo jela au faini.

Akifungua mafunzo ya sheria hiyo kwa wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini, Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimali Watu Serikalini, Ibrahim Mahumi, alisema viongozi hao wanapaswa kutambua sheria ipo na imeanza kufanya kazi. "Hatutarajii kuona mkuu wa taasisi kuingia mgogoro na serikali kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema awali kuna mambo yaliyokuwa yanaagizwa na Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) yalikuwa hayatekelezwi kutokana na kutokuwapo na nguvu kisheria lakini kwa sasa sheria ipo na utekelezaji umesisitizwa.

"Hivyo mtu yeyote kama ilivyo kwenye sheria nyingine, ukiacha kutekeleza kinachoelekezwa na sheria, utapambana na sheria hiyo hiyo," alisema.

Mahumi alisema eneo la serikali mtandao halikuwa na sheria mahsusi ambayo ilikuwa inaongoza matumizi ya TEHAMA lakini mwaka jana serikali ilitunga sheria hiyo ili kurahisisha kutoa mwongozo namna ya kutekeleza serikali mtandao.

"Sheria hii ilikuja kutokana na vikwazo vingi vya kiutendaji, kisera na kisheria ndiyo maana serikali imetengeneza sheria hii mahsusi ili kutatua tatizo hili," alisema.

Alisema wakati kulipokuwa na tatizo kwenye utendaji hapakuwa na sheria mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa serikali mtandao. Aidha, alisema sheria hiyo inahitaji kueleweka kwa wadau wote wakiwemo Wakuu hao wa idara na vitengo na baada ya mafunzo hayo watakuwa ni mabalozi kwenye taasisi na wadau mbalimbali ili kufahamu kwa undani sheria hiyo. "Tunaamini baada ya mafunzo haya tatizo la kimiundombinu, mifumo na kwenye utumiaji wa TEHAMA zitatatuliwa,"alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Dk. Jabiri Bakari, aliziasa taasisi hizo kuzingatia sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao wakati wa kusanifu, kujenga na kuendesha mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

Alisema kuwa uzingatiaji wa sheria hiyo kanuni zake utasaidia matumizi sahihi ya TEHAMA.



Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ngóndi akitoa salamu kwa washiriki wa mkutano wa kujadili utekelezaji wa mkakati wa kutokomeza mauaji ya wazee uliofanyika jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya – Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii ambaye pia ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Sayi Magesa na Mwakilishi kutoka TAMISEMI, Mariam Mkumbwa. **PICHA: WAMJW**

# Tanzania, Afrika Kusini zaunda kamati ya kuratibu ushirikiano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA na Afrika Kusini zimeunda kamati ya pamoja yenye wajumbe kutoka nchi hizo ili kushirikiana katika kutekeleza hati ya makubaliano (MoU) kwenye masuala ya viwanda, biashara na uwekezaji.

Hatua hiyo ilifikiwa jana jijini hapa katika kikao cha pamoja kati ya Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ally Gugu, na ujumbe kutoka Ubalozi wa Afrika Kusini nchini Tanzania.

Akizungumza na ujumbe huo, Gugu alisema nchi hizo zimekuwa na ushirikiano wa kibiashara, kiuchumi na kisiasa kwa muda mrefu tangu kipindi cha kudai uhuru.

"Hivyo ni jambo jema kushirikiana katika kuendeleza biashara kati ya nchi hizi mbili, na ushirikiano huu umezidi kuimarika kwa uwapo wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Nchi hizi mbili zilikubaliana kuwa na hati ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya viwanda na biashara," alisema.

Alisema lengo la hati hiyo ni kuimarisha uhusiano wa kibiashara zaidi kwa kuongeza biashara kwa maslahi ya pande zote mbili hasa ikizingatiwa Afrika Kusini ni moja ya nchi vinara katika uwekezaji barani Afrika.

Naye Kaimu Balozi wa Afrika Kusini nchini, Sizwe Mayoli, alisema amefurahi kupata fursa ya kujadili masuala ya ushirikiano wa kiuchumi, kibiashara na uwekezaji baina ya Tanzania na nchi yake katika kikao hicho.

Alisema baadhi ya masuala yaliyojadiliwa katika kikao hicho ni pamoja na kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa hati hiyo ya ushirikiano katika sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji.

"MoU hii inatoa fursa ya kuunda kamati ya pamoja ya biashara na uwekezaji katika nchi hizi mbili, hivyo kikao chetu kimehitimishwa kwa kuunda kamati hii ili kushirikiana pamoja katika kutekeleza hati ya makubaliano," alisema.

# TAKUKURU, TFC kuboresha ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, zimejipanga kuimarisha na kuboresha sekta ya ushirika nchini ili kuondokana na kero zinazoikabili sekta hiyo.

Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa kutoka TAKUKURU, Sabina Seja, aliyasema hayo jana jijini hapa katika kikao cha kujadili uchambuzi wa mfumo wa utendaji wa vyama vya ushirika kutokana na utafiti iliyofanywa na taasisi hizo.

Alisema taasisi hiyo imechukua hatua hiyo ya ushirikiano ili kuokoa mali za ushirika pamoja na kuimarisha utawala bora.

Mkurugenzi huyo alisema utafiti huo utasaidia kutathmini utendaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika wa mazao kwa kubainisha maeneo yenye viashiria vya rushwa ili kupendekeza namna bora ya kuimarisha mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa vyama hivyo.

Aidha, alisema baadhi ya maeneo mahususi yaliyozingatiwa katika utafiti huo ni pamoja na kutathmini mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa ushirika wa mazao, kutathmini ufanisi wa mifumo ya ndani na kubainisha mianya ya rushwa katika utendaji wa vyama hivyo.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu, Dk. Benson Ndiege, alisema tume itaendelea kushirikiana na wadau katika kuimarisha na kuhakikisha kuwa ushirika unaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu za ushirika.


Mrajis aliongeza kuwa mfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika utaimarishwa kwa kuzingatia masuala mbalimbali ikiwamo kuangalia sifa za watendaji wa vyama, taratibu za uendeshaji wa mikutano ya wanachama pamoja na utoaji wa huduma kwa wanachama.

"Ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika kuimarisha utawala bora kwenye Vyama vya Ushirika ni vizuri kuendelea kuangalia kwa karibu zaidi namna mifumo ya udhibiti ya ndani inayohusisha mambo mengi kama vile usomaji wa taarifa za fedha, ukaguzi wa vyama," alisema.

Mrajis alisema baadhi ya kero zilizobainika katika utafiti huo ni pamoja na uelewa mdogo wa masuala ya uendeshaji na usimamizi wa Ushirika kwa watendaji pamoja na wanachama wa Ushirika.

"Hivyo utafiti huu pamoja na majadiliano ya kikao hicho yalipendekeza kuongeza utoaji wa elimu ya ushirika kupitia njia mbalimbali ikiwamo matumizi ya vyombo vya Habari,"alisema.

Kikao Kazi hicho kimehudhuriwa na Wadau mbalimbali wa Ushirika Ikiwemo Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na TFC.



# Mgombea ajinadi kukuza uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Democratic Party (DP), Shafi Hassan Suleiman, amewataka wananchi wa Zanzibar kumpa ridhaa ili kuyatumia maeneo huru ya uchumi ya Micheweni, Pemba na Fumba, Unguja kwa uwekezaji na kuzalisha ajira.

Akizungumza na wananchi na wafuasi wa chama hicho katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni Sebleni, Unguja, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeyatenga maeneo huru ya uchumi likiwamo la Micheweni tangu mwaka 1992 bila kuyatumia.

"Nikichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar nakusudia kuyatumia maeneo huru ya uchumi ya Micheweni, Pemba, kwa kujenga viwanda vikubwa vitakavyozalisha ajira," alisema.

Pia aliwataka wananchi kudumisha amani na utulivu katika kipindi chote ili taifa liwe na utulivu kabla na baada ya uchaguzi.

Alisema Wazanzibari wamechoka na vurugu za kisiasa zinazojitokeza kipindi cha uchaguzi mkuu na kuwaweka wananchi katika hofu na wasiwasi mkubwa.

"Chama cha DP kinawataka wanachama na wafuasi wake kuwa watulivu katika kipindi hichi kuelekea uchaguzi. Msikubali kurubuniwa kushiriki katika vurugu za kisiasa zinazotokana na jazba," alisema.

Naye Mgombea mwenza wa chama hicho, Zaina Juma Khamis, aliwataka wananchi wajenge matumaini makubwa kwa chama chao ambacho kimejipanga kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

"Wananchi mkituchaguwa matarajio yetu makubwa ni kuharakisha maendeleo kwa wananchi na kuongeza ajira katika miradi mikubwa," alisema.

# Wavuvi wamwomba Dk. Mwinyi kuwajali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAVUVI wa Zanzibar wamemtaka mgombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, endapo atachaguliwa, kuimarisha sekta ya uvuvi ili kukuza ucuhumi.

Wakizungumza na mgombea huyo katika kampeni zake za kisayansi zinazoendelea kwa kukutana na makundi mbalimbali, wavuvi hao walisema kuwa wanadharaulika katika jamii kutokana na hali zao duni za kiuchumi.

Akizungumza kwa niaba ya wavuvi wezake, Katibu wa Wavuvi kutoka Kijiji cha Chwaka, Ali Salum Nassor, alisema lazima wavuvi wawekewe masoko makubwa kila wilaya ili kuuza samaki wao kwa bei ambayo itawanufaisha wavuvi.

"Mheshimiwa mgombea, sisi wavuvi hata tunapotaka kutafuta mke tunapoenda kuposa tunajadiliwa kutokana na hali zetu duni za kiuchumi," alisema.

Alisema wavuvi wa Zanzibar wanategemea zaidi masoko mawili makuu ambayo ni Soko la Darajani na Malindi, hivyo samaki wanapokuwa wengi soko la samaki hushuka na huuza kwa bei ya kutupa.

Pia alisema wavuvi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki jambo ambalo limesababisha kushindwa kufika katika bahari kuu kuvua samaki na kuishia katika maji madogo.

"Tunasikitishwa sana samaki waliopo katika bahari kuu wanavuliwa na wavuvi kutoka nje ya nchi kwa sababu wao hawana uwezo wa kufika huko," alisema.

Naye mvuvi Idi Omar Khamis kutoka bandari ya Forodhani, alitaka wavuvi kuwezeshwa kutokana na hali ya mazingira yao na vitendea kazi vyao ni dhaifu.

Alisema wanahitaji zana za kisasa za kufanyia kazi ya Uvuvi na kuwepo kwa Viwanda vya kusindika samaki ili kukuza kipato chao.

"Ukipata ridhaa ya kuwa Rais wa Zanzibar tunakuomba usimamie uvuvi haramu ambao unachafua mazingira ya bahari na pia iundwe Wizara pekee ya uvuvi kwa sababu sekta hii imebeba ajira nyingi," alisema.

Kutokana na maombi hayo, Dk. Mwinyi alisema akichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar anakusudia kuimarisha sekta hiyo kwa kuwawezesha wavuvi kuingia katika uvuvi wa bahari kuu wenye tija ili kuvuna hazina ya rasilimali ya viumbe vya baharini.

Alisema sekta ya uvuvi bado haijawakomboa wavuvi wa Zanzibar ambao wanavua kwa kutumia zana duni ambazo hazina tija licha ya Zanzibar kuzungukwa na bahari.

"Nikichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar nakusudia kuimarisha sekta ya uvuvi wa bahari kuu pamoja na uvuvi wa maji madogo na ule wa ufugaji wa samaki ili uwawezeshe wavuvi kupata kipato kikubwa. Hata mtakapokwenda kuposa jamii isiwajadili kutokana na kazi yenu hii ya uvuvi, alisema.

Pia alisema serikali atakayoiongoza itajenga viwanda vya kusindika samaki ambavyo vitasaidia kuongeza thamani na kuwawezesha wavuvi kupata kipato kikubwa.

Alisema atawakaribisha na kufungua milango kwa wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya samaki ili kuongeza uzalishaji.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi Mdogo wa China anayefanyia Kazi zake Zanzibar, Xie Xiaowu, alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kwa mazungumzo na kuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi.
**PICHA: IKULU**

# Dk. Shein azitaka serikali, sekta binafsi kuzidi kukuza biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka sekta binafsi kuendelea kushirikiana na Serikali katika kukuza sekta ya biashara, ambayo hivi sasa inaendeshwa kupitia sekta hiyo.

Dk. Shein aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa jengo la Sheikh Thabit Kombo (Thabit Kombo Building), lililojengwa kwa ushirikiano kati Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Alisema katika kufanikisha dhamira hiyo serikali ya Zanzibar itaendelea kuimarisha mazingira ya kuendesha shughuli za kibiashara na kukuza uwekezaji.

Pia aliwataka wananchi kufanya kazi kwa bidii na kujiamini kwa kuelewa kuwa mafanikio yatapatikana kupitia wananchi wenyewe.

Alisema Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 pamoja na Ilani mpya ya 2020- 2025, zimesisitiza uimarishaji wa sekta ya utalii, biashara na usafirishaji, ambayo yameshughulikiwa kwa jitihada kubwa na kupata mafanikio katika utekelezaji wake. Rais Shein alisema amefarijika kuona ufunguzi wa maduka katika eneo la Michenzani na kuunasibisha ujenzi wa jengo hilo na dhana iliyoelezwa na mwekezaji wa Kimarekani Tom Freston, inayosema 'ubunifu ni kuchukua vitu viwili vilivyopo na kuviweka pamoja kwa njia mpya'.

Alisema ZSSF imetumia ardhi ndogo ya mahali hapo iliyokuwa ikitumika kwa shughuli tofauti, ikiwamo biashara na kujenga jengo moja kubwa la ghorofa linalopendeza ambalo ndani yake kuna maduka ya kisasa ya biashara.

Hatua hiyo, alisema pia imeipatia maskani maarufu ya CCM Kisonge sehemu za ofisi zenye haiba, akibainisha kuwa huo ni ubunifu unaolingana na wakati.

Alisema ni vyema masuala ya maendeleo yakazingatia wakati ili kufikia mafanikio na kuwanasihi wananchi wanaopata fursa katika nyanja za uwekezaji (ikiwemo ujenzi) kuwa tayari kutoa maeneo yao ili kufaidika na vitu vizuri na vilivyo bora zikiwamo rasilimali za majengo na kuwataka kuacha kukataa mambo mapya yenye tija.

Dk. Shein aliwataka wananchi na wanachama wa CCM kuielewa na kuiunga mkono kwa uzalendo mkubwa dhamira ya chama hicho katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Alisema Serikali inalenga kuendelea kuliimarisha eneo la Michenzani kibiashara kwa kujenga eneo la kuegesha magari, hivyo kuongeza idadi ya wafanyabiashara, hatua itakayotoa majibu sahihi dhidi ya wale wote waliokuwa wakibeza azma ya ujenzi huo.

Kuhusu uchaguzi mkuu, Dk. Shein alivitaka vyama vya siasa na wananchi kuendelea kufanya kampeni zao kwa njia za kistaarabu, na kujenga imani na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Aliwataka Wazanzibar kuwa watulivu kwa kigezo kuwa ndiyo njia pekee ya kupata viongozi bora pamoja na kusema serikali haitakuwa tayari kuona kunatokea vurugu.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema wajibu wa ZSSF hauko kwa wanachama wake pekee bali ni kwa jamii yote ya Wazanzibari.

Alisema hatua ya ZSSF kuingia ubia na CCM ni jambo zuri kwa kuzingatia CCM ni chama chenye nguvu na kinachoaminika muda wote, sambamba na kufanya mambo yenye manufaa kwa wananchi wake.



GABO
UKURASA 12

JUMAMOSI SEPTEMBA 26, 2020





## 'WANANIKIMBIA'

# Chemical analia, wao wanamtega

WIKI hii, rapa maarufu nchini, Chemical, ameibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii, baada ya kutoa kilio chake kwamba wanaume wanamkimbia.

Katika akaunti yake ya Instagram, Chemical, aliweka ujumbe akiomba ushauri kutokana tatizo la kukosa wanaume wa kutaka kumuoa, licha ya umri wake kuzidi kusonga mbele.

Ujumbe huo ambao baadhi wanaona kama utani, lakini wachambuzi wa watu maarufu, wanasema Chemical anaweza kuwa na kitu moyoni mwake, hivyo kuandika ujumbe huo sawa na kutema sumu inayomuumiza.

Wanasema, kile kilichoandikwa kinashabihiana na maumivu aliyonayo moyoni.

"Unajua Chemical tofauti na wasanii wengine wa kike, licha ya kuwa na wajihi wa kike lakini mitindo na jinsi anavyojiweka inawatia mashaka wanaume," amesema Shabani Hamza.

Hata hivyo, Hamza, ameeleza wasichana wenye muonekano kama Chemical, wako wengi na wamefanikiwa kuolewa na kupata watoto.

"Ujumbe wake unaweza kushabihi maumivu ya moyoni mwake, lakini namshauri kuwa na subira na kuangalia nini anaweza kufanya kuwavutia wanaume wenye nia ya kuoa," ameshauri.

Katika chapisho lake, msanii huyo alisema anajiona kama hana bahati kwani kila wanaume anayetaka kuwa naye kwenye mahusiano anamkataa.

"Wana wa Insta, Nipo hapa mbele yenu kuomba ushauri serious, nikisema nitajioa sio kwamba napenda, ila mwenzenu sina bahati jamani, nishatongoza sana ila wanaume msivyo na huruma hamuogopi kunikataa, najua sivutii kihivyoo ila mgeni huruma basi, hata wale wa kuja na kupita tu nitaridhika"

BASI SAWA

## Kanumba azidi kumtisha Gabo

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Gabo Zigamba, amejaribu kufafanua kwa nini watu hufananisha ukuaji wa tasnia hiyo na kifo cha Steven Kanumba.

Akizungumza na EATV, Gabo, amesema ni kosa kufananisha jambo hilo kwa sababu ubora wa tasnia upo palepale pamoja na marehemu Kanumba kukosekana.

"Tasnia ni kubwa sana ikifananishwa na marehemu Kanumba, watu watakuwa wanakosea kwa sababu tatizo lililokuwapo ni uchache zinazoonekana, lakini kingine ni sehemu za kutolea kazi, usambazaji na ujumbe umekuwa shida sana" alisema.





## Shilole awadatisha watu

NI kweli mwanamuziki na mjasiriamali, Shilole, anatoka kimapenzi na kijana mbichi?

Swali hilo linazidi kuwaumiza watu katika mitandao ya kijamii, baada ya kumuona msanii huyo akiwa karibu na mpiga picha wake anayefahamika kama Rommy.

Wawili hao walishea kwenye mtandao wa Instagram ikiwaonyesha wakiwa wote katika mikao yenye utata inayoashiria kuna jambo zaidi kati yao.

Hata hivyo, Rommy, amejitetea kwamba hana uhusiano wa kimapenzi na Shilole, ila ukaribu wao unatokana na kazi pekee, hivyo watu wasianze kufikiria jambo ambalo halipo.





## Jitu Baya kaleta 'I Won't you' kiaina

RAPA anayekuja kwa kazi, Jitu Baya, amekamilisha ngoma yake mpya inayoitwa 'I Won't You' ambayo amemshirikisha Cade Lana.

Akizungumza na BT, Jitu Baya amesema ngoma hiyo iliyorekodiwa katika studio ya Fresh Boy, imeanza kusikika katika vituo mbalimbali vya redio pamoja na mtandao wa You Tube.

Amesema hivi karibuni watakamilisha video ya wimbo huo, kazi ya uchukuaji wa picha umekamilika na wakati wowote itatambulishwa rasmi.

## Mali ya urithi: Urithi wenye laana

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo wa kiswahili unaosema 'mali ya urithi haina baraka.' Wenye msemo huu hawana maana kuwa kila kinachoachwa na wazazi kinatoweka haraka kama hakuna msimamizi.

Kila binadamu anarithi mali za wazazi, lakini hutakiwi kuitegemea kwenye maisha yako.

Inapotokea hivyo, ndipo mwanzo wa matatizo mengi ya ugomvi, na tafrani kwenye familia.

Leo tunaiangalia filamu isemayo 'Mali ya Urithi.'

Wahusika wakuu kwenye filamu hii ni Tini White na Ringo.

Inaanza kuonyesha kwenye msiba, ambapo Tini na Ringo wamefiwa na kaka yao Ngondo.

Kaka yao huyo ndiye aliyeachiwa mali zote na marehemu baba yao. Katika usia wake wa mdomo na maandishi walimwambia Ngondo kuwa mali hizo ni za wote, lakini yeye ndiye asimamie kitu pamoja na kukaa hati za nyumba na mashamba.

Marehemu aliacha nyumba moja kubwa na mashamba matatu. Na aliusia visiuzwe.

Lakini baada ya Ngondo kufariki, Tini na Ringo wakataka nyumba na mashamba yauzwe kwa sababu wao wasingeweza kuziendesha mali hizo kama ilivyokuwa kwa kaka yao.




Hata hivyo, wakati anafariki Ngondo, hati zilikuwa kwa mkewe na mwanasheria.

Mwanasheria aliwaambia Ringo na Tini kuwa usiwa na marehemu baba yao na hata wa kaka yao ni kwamba mali hizo zitaendelea kuwapo na wao watazitumia tu na haziruhusiwi kuuzwa.

Uamuzi huu haikuwapendeza, hivyo walitaka kuiuza nyumba kwa siri. Akatafutwa dalali akapatikana. Akatafutwa mteja naye kapatikana.

Akatembezwa kwenye nyumba hiyo ya vyumba sita wakati shemeji yao hayupo. Kilichotokea ni kwamba dalali alipigwa vibao na mtu ambaye hajulikani na nani.

Dalali akatimua mbio hadi nyumbani kwake, akajivua na udalali wenyewe. Mteja na mkewe kuona hivyo nao wakaingia ndani ya gari lao na kuondoka haraka. Kwa bahati nzuri bado walikuwa hawajatoa fedha.

Tini na Ringo walipoambiwa, moja kwa moja wao wakapeleka shutuma kwa shemeji yao, mke wa marehemu kaka yao kuwa ni mchawi na anachotaka kukifanya ni kuwanyang'anya mali yao.

Wakaenda kwa mganga ambaye aliwaongopea na kuwapa dawa za uongo.

Walichofanya sasa ni kufanya vituko vinavyoashiriwa uchawi ili mradi tu kumroga shemeji yao ambaye aliapa kuwa hawezi kuwapa hati kwa sababu aliagizwa kuwa mali ile isiuzwe, bali itumiwe na wanafamilia.

Ringo na Tini wakawa wataka kutumia nguvu ili kuuza nyumba. Kilichotokea ni kwamba mnunuzi na wao wenyewe walipigwa makofi na mtu au watu wasiojulikana kila wanapofika na kuingia kwenye nyumba hiyo kwa nia ya kuiuza.

Cha ajabu ni kwamba ndani humo analala shemeji yao na hapigwi na mtu yoyote.

Kilichokuja kugundulika ni kwamba kilichokuwa kikiwapiga, kila mtu aliyekuwa na wazo la kutaka kuuza, kudalalia au kununua walikula vibao na mtu asiyejulikana.

Walitimua mbio kila mtu na njia yake. Kilichokuja kugundulika kwa kwamba mzimu wa baba na kaka yao ndiyo uliokuwa unafanya kazi ya kulinda nyumba ile isiuzwe, pamoja na mali zingine.

Biashara ikafa hapo hapo, mali ikabaki kuwa na familia, kila mtu atumie, lakini zisiuzwe kizazi kwa kizazi.





## Giny aanza kuwatishia nyau wakongwe

MWANAMUZIKI chipukizi wa Bongo Fleva, Joshen Adam, maarufu kama 'Giny' amesema kazi yake mpya 'Jini Baba' italeta hofu kwa wasanii wakubwa.

Akizungumza na BT, Giny, amesema ameshindwa kutambulisha mapema kama alivyoahidi kutokana na kufuata ushauri wa watu wanamuongoza ambao wanataka ngoma hiyo kuleta mtikisikiko mkubwa.

"Nilipanga ngoma yangu kutambulisha mwezi huu, lakini kutokana na ukubwa wa wimbo wenyewe na aina ya muziki wake, kila mtu na hasa viongozi wangu wanashauri nitambulishe kwa ukubwa unaolingana na kazi yangu," amesema,

## ZILIRUDIWA STUDIO ZIKABAMBA TENA

**Na Adam Fungamwango**

SIKU hizi kumekuwa na studio nyingi kiasi kwamba wanamuziki na wasanii wengi wamekuwa wanachagua wapi waende kurekodi.

Na wakati mwingine imesababisha kusiwe na udhibiti wa maneno makali kutoka kwa baadhi ya wasanii ambao baadhi ya ngoma zao zimekuwa zina lugha ya ukakasi, kiasi kwamba wakati mwingine mtu anashinda kukaa na watoto wake au watu anaowaheshimu kama wakwe kusikiliza wimbo.

Zamani kulikuwa na studio moja tu Redio Tanzania Dar es Salaam, ambayo ilikuwa ikitumika kurekodi nyimbo za bendi zote nchini.

Lakini kabla ya kurekodi, bendi husika ililazimika kupeleka maneno au mashairi ya nyimbo wanazotaka kurekodi.

Likishafanyika hilo kuna jopo linakaa na kupitia maneno ya wimbo mmoja baada ya mwingine.

Kama yakiwa hayana matatizo sawa, lakini jopo hilo likishagundua kuwa kuna maneno yasiyofaa kwa sababu mbalimbali za kijamii, kidiplomasia, kulinda umoja ya kitaifa, au kibiashara, basi hufuta maneno hayo.

Jopo hilo ambalo huwa na watangazaji wenye ufahamu wa muziki, baada ya kufuta hupendekeza maneno mbadala kutumika au kushauri bendi na kundi kutafuta neno mbadala ambalo linaweza kupachikwa na kutoleta athali yoyote kwenye mapigo au 'taiming' ya muziki, yaani lisizidi au kupungua urefu kutokana na mpangilio wenyewe wa muziki.

Leo tutaziangalia nyimbo za zamani ambazo zina baadhi ya maneno ambayo yalirekebishwa studio na bendi kulazimika kubadilisha maneno, lakini bado wimbo ukawa mzuri na maana ile ile, huku wengi wakiwa hawajui nini kilitokea.

**Rangi ya Chungwa-Nyanyembe Jazz**

Huu ni wimbo maarufu zaidi unaopendwa na vizazi vyote. Huwezi kupita kwenye baa au kumbi zinazopiga muziki wa laivu usipigwe wimbo huu. Ambacho wengi hawakijui awali wimbo huu uliitwa 'Rangi ya Fanta'. Ulitungwa na kuimbwa na bendi ya Nyanyambe Jazz ya Tabora.

Na kwenye kuimba waimbaji waliimba 'Najuta, ni kinda langu ni lenye rangi ya Fanta.'

Kilichofanya ubadilishwe hapo ni sababu tu za kibiashara, ndipo ukabadilishwa hapo hapo studio wakati wa kurekodi, wakaimbwa 'Najuta ni kinda langu ni lenye rangi ya Chungwa.'

**Ngapulila-Vijana Jazz**

Ngapulila ni wimbo maarufu sana uliotamba katikati ya miaka ya '80, ukipigwa na Vijana Jazz Band.

Waliokuwa wanakwenda kwenye kumbi ambazo bendi hiyo inapiga, watakwambia kuwa kuna sehemu ambayo anaimba Hemed Maneti "Ngapulila, mwenzio kashikwa ughaibuni, kazamia meli na kukuywa na madawa ya kulevya na sasa yupo kifungoni."

Ile sehemu ilibadilishwa, kwani kwenye kumbi kwenye neno ughaibuni halikuwepo, badala yake iliimbwa "mwenzio kashikwa Pakistan." Nadhani neno lilibadilishwa studio kwa sababu za kidiplomasia.

**Kipini cha dhahabu-Biashara Jazz**

Ni wimbo uliokuwa unawaasa akinadada wanaopenda vitu vya gharama na anasa zisizo na msingi.

Biashara Jazz walitunga wimbo huu mwanzoni mwa miaka ya '80 na kuna sehemu inaimbwa "Mara anataka kiatu cha ghorofa, manukato kipini cha dhahabu, na nywele za bandia na khanga za mpunga wa kisele..."

Hapo kwenye khanga, awali mwimbaji alitaja 'khanga za Mombasa', lakini ilibadilishwa hapo hapo studio kwa madai ya kutangaza biashara za Tanzania na si za nje ya nchi. Khanga za Mpunga wa Kisele zilitengezwa Bongo na za Mombasa nchini Kenya.

**Kaka Mahmoud-Juwata Jazz**

Ni wimbo ambao una maudhui ya mtu aliyempenda msichana kwenda dansi, lakini dada huyo akamtaka jamaa wakutane kesho yake sehemu fulani ili ampe jibu lake. Awali Msondo waliimba kuwa dada huyo alimtaka wakutane maeneo ya Polisi Ufundi. Lakini wimbo ulipofika studio, walitakiwa wabadilishe jina, wasiliite hivyo kwa sababu kuna neno la Polisi. Lakini kwa sababu maeneo hayo ni Keko Machungwa, basi ikaimbwa 'tukutane Keko Machungwa.'

**Teddy-Vijana Jazz**

Hii ilikuwa ni Vijana Jazz ya akina Mohamed Salum 'Gotagota' ambayo ilikuwa ni mwisho kabla haijapoteza umaarufu wake. 'Teddy' ni wimbo uliomhusu mke aliyekuwa anamuaga mumewe kuwa anakwenda ngomani, lakini hafiki. Anakwenda akakokujua mwenyewe. Vijana waliimba kuwa anayemdanganya ni shoga yake mmoja ambaye hapa mjini anaitwa 'shangingi'. Wakiwa studio za RTD, waliambiwa waondoe neno hilo na



Eddy Sheggy

# Kanye, Kim kimenuka vibaya



KAMA ni kweli, basi ni sawa na tetemeko! Kwani taarifa zinazovuma mitandaoni ni staa wa vipindi vya televisheni, Kim Kardashian na mumewe, Kanye West, hawapo vizuri na wakati wowote wanaweza kupeana talaka.

Kulingana na mtandao wa PageSix, rapa huyo ambaye ni maarufu duniani, ameonekana kuchanganyikiwa baada ya mkewe kuonekana yupo katika mkakati wa kuomba talaka.

"Kim anapanga kuomba talaka, lakini anasubiri mumewe kuanza rasmi kwa msimu mpya," kilisema chanzo hicho.

Kanye West na mkewe, Kim Kardashian, walifunga ndoa mwaka 2014, na wamebahatika kupata watoto wanne.



## Cardi B ukisikia mapenzi upofu 'ndo' hayo

RAPA mkali kutoka Marekani, Cardi B, ametupilia mbali uvumi ulioenea katika mitandao ya kijamii kuwa anataka kumtaliki mume wake baada ya kugundua anatarajia kupata mtoto na mwanamke mwingine.

Akizungumza mapema wiki hii, Card B, amesema mume wake Offset, hatarajii kupata mtoto kama inavyoenezwa na watu, na kwamba yeye hana mpango wa kuomba talaka.

"Hana mtoto wmingine, hakuna mtoto yupo njiani. Uvumi huu ni uongo, Card B anafikiria watoto wake na kila kitu kiende kama alivyopanga,"kilisema chanzo hicho.

## Yemi Alade kumbe hupendi kuona uonevu!

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Yemi Alade, amewajia juu baadhi ya watu wenye tabia ya kuwalaumu wanawake, endapo mwanaume wake atatoka nje kimapenzi.

Kulingana na ujumbe wake katika ukurasa wake wa Twitter, Alade, amesem haijalishi mema anayofanya, lakini ikitokea tatizo hilo mwanamke huwa wa kwanza kuonyeshwa vidole.

"Watu wasifanye haya, haijalishi mambo gani mema amefanya, hakika hakuna aliyekamilika lakini kutoka nje sio jambo la bahati mbaya,"amesema.






## BB Naija: Washiriki washikana uchawi hadharani

WAKATI shindano la Big Brother Nigeria, linazidi kushika kasi, ndani ya nyumba mambo yanazidi kuwaka moto na safari hii washiriki wameanza kushikana uchawi.

Wiki hii, mmoja wa washiriki, Vee, ameweka wazi kwa kumfananisha Ozo sawa na shetani kwa kile anachodai, mshishiriki mwenzake huyo anataka yeye atolewe ndani ya nyumba hiyo.

Vee, wakati akizungumza na Neo, alisema anaamini Ozo, anafanya mkakati ili aishie njiani haraka.

Kutokana na hali hiyo, Vee alimfananisha mwenzake sawa na wakala wa shetani, hivyo anakuwa makini naye kila wakati.

## Ushebebe sijui kama vijana wamekuelewa

MSANII maarufu wa uchekeshaji kutoka Nigeria, Ushebebe, ametoa wito kwa vijana wa kiume kuwa na tabia ya kuweka akiba ya fedha kabla ya kuamua kuoa.

Ushebebe, amesema mwanaume akianza kuwa na fedha ana uwezo wa kusimamisha masuala mengi ambayo haya msingi katika maisha.

Mchekeshaji huyo, amesema ni muhimu vijana kuishi peke yake, kuliko kukimbilia kuoa mwanamke ambaye anatoka katika familia maskini.



MAKALA

# NEC, wadau wa uchaguzi mmeyasikia ya walemavu?

**Na Gaudensia Mngumi**

UCHAGUZI Mkuu kuwapata wabunge, madiwani, wawakilishi na marais ndiyo habari ya mjini. Watanzania wanaingoja kwa hamu Jumatano Oktoba 28, ili kutimiza takwa la kidemokrasia la kujichagulia wawakilishi na viongozi.

Washiriki wa uchaguzi huo ni wengi lakini siku hiyo ikiwalenga zaidi wapigakura. Miongoni mwa wadau wa kura hizo ni wahitaji, hawa ni watu wenye ulemavu ambao nao ni sehemu ya washiriki.

Ili kufahamu maoni ya wahitaji hao hasa walemavu wasioona, Nipashe inazungumza na Mratibu wa Ukuzaji Mitaala na Upimaji katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ELIGIUS BWALIYA, mlemavu wa macho na viungo, kujua hisia za watu wenye uhitaji maalumu wakati huu wa kampeni kuelekea uchaguzi mkuu...

SWALI: Ni nini maoni yako katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushiriki bora wa walemavu kwenye uchaguzi mkuu wa 2020?

JIBU: Ili watu wenye ulemavu waweze kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

Mosi ni vyema kuwa na elimu ya mpigakura: kama ilivyo kwa watu wengine wasiyo na ulemavu. Ikumbukwe wenye ulemavu pia wanastahili kupewa elimu ya mpigakura ambayo itamsaidia kujua nini cha kufanya na wajibu wake katika kushiriki uchaguzi.

Jambo jingine ni kuwapo hamasa watu wenye ulemavu wanatakiwa kuhamasishwa ili kushiriki kikamilifu katika uchaguzi kwani wengi wao wamekata tamaa na kuona kuwa hata wasiposhiriki hakuna wanachopoteza.

Wanaamini hivyo kwa kuwa viongozi wengi hawatoi kipaumbele katika kuyashughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. Wengi wanaamini kuwa mambo ya msingi yanayowahusu wenye uhitaji maalumu wakiwamo wasioona hayazungumziwi.

Nitoe mfano masuala ya kodi, afya, na pia kusahaulika katika vyombo vingi vya uamuzi na katika nafasi mbalimbali za uteuzi kama wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na taasisi mbalimbali za kiserikali.

Ukweli ni kwamba nafasi za uteuzi ni nyingi kiasi kwamba ingependeza angalau kwa kila nafasi ya uteuzi kuwe na mwenye ulemavu kama ilivyo kwa wanawake kwani saikolojia ya jamii inawaweka walemavu, wanawake, wakimbizi, watoto na wazee katika kundi moja.

Hawa jamii inawaona kuwa ni 'disadvantaged group' ila kwa sasa wanawake wamepiga hatua kwa kuwa kuna vyombo na taasisi nyingi zinazopaza sauti juu yao.



Mratibu wa Ukuzaji na Tathimini ya Mitaala wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Eligius Bwalya. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

SWALI: Kuna madai kuwa kukosekana ulinzi hasa kwa wenye ulemavu kunawakwamisha kushiriki uchaguzi, hilo unalizungumziaje?

JIBU: Uhakika wa usalama ni suala la msingi.Imezoeleka kuwa katika mikutano mingi ya kisiasa kuna matukio ambayo kwa watu wenye ulemavu ni kikwazo kikubwa.

Kikwazo hicho wakati mwingine kikawakwamisha kushindwa kuhudhuria hata mikutano ya kampeni na hatimaye kutoshiriki uchaguzi ipasavyo.

Hivyo niseme licha ya kwamba wanapenda kuhakikishiwa ulinzi na usalama kwa kuwa yanapotokea machafuko au fujo, waathirika wakubwa mara nyingi ni pamoja na watu wenye ulemavu. Hilo linaweza kuwa tatizo kwa makundi mengi ya walemavu wakiwamo wa viungo, viziwi na wasioona.

SWALI:Vipi kuhusu masuala ya mawasiliano ya habari?

JIBU: Changamoto ya mawasiliano na upatikanaji wa habari nalo ni muhimu kulizungumzia wakati huu wa kampeni za uchaguzi mkuu,

Ni dhahiri kuwa kundi la watu wenye ulemavu hupata taarifa kwa njia chache mno na mara nyingine haziwafikii, kikamilifu wala hawazipatika kabisa.

Kwa mfano, viziwi hawana fursa ya kupata taarifa kwa wakati na kwa usahihi kwa kukosekana lugha za alama na wakalimani katika matukio muhimu.

"Hebu tazama kampeni zinazoendelea, sera na ahadi zinazoongelewa au kuzungumzwa majukwaani zinawafikia viziwi au viziwi bubu kwa wakati na kwa usahihi? Kwa wasioona hutegemea redio kwa kiasi kikubwa kupata habari na ndiyo maana kama kuna kitu ambacho wasioona wanalalamika ni hatua ya Wiziri ya Habari na Sanaa kupiga marufuku kusoma magazeti kwa kina bila kutoa njia mbadala ya watu hawa kupata taarifa ya kinachoendelea nchini na duniani kwa ujumla."

Aidha, matangazo mengine yanatolewa kwenye vyombo vya habari, mathalani runinga utasikia kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba hizo, kwa 'email' au anuani yote haya kama yanaandikwa kwenye runinga asiyeona hawezi kutambua.

SWALI: Watu wenye uhitaji maalum hasa walemavu wamezungumzia suala la vifaa, safari hii kuna mabadiliko?

JIBU: Vifaa: Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), mara kwa mara wamekuwa wakisikika wakisema kuwa kutakuwa na vifaa vinavyomwezesha mlemavu kupiga kura mwenyewe bila kuhitaji usaidizi wa mtu mwingine.

"Jambo hili limekuwa likisemwa kisiasa kwani mara zote wanaposema hivyo mpigakura mwenye uhitaji huoni uhalisia na ukweli wa taarifa hiyo. "

Fanya uchunguzi au utafiti kwa baadhi ya walemavu na hasa wasioona na wasio na mikono, kisha uwaulize iwapo mara zote wanapoambiwa kuna mazingira rafiki kwa walemavu walishawahi kupiga kura wenyewe bila usaidizi wa mtu mwingine?

Jambo hili limefanya suala la kupiga kura si la siri tena kwa walemavu. Ni kwa sababu aliyemsaidia anafahamu kuwa kampigia nani.

Pengine katika mchakato huo mlemavu asiyeona hakufahamu kama maelezo yake aliyotoa kwa anayemsaidia yalitekelezwa kama alivyotaka, au aliyemsaidia alifanya kila anachipenda.

Changamoto kama hizo pia zinawakatisha tamaa walemavu.

Ushauri wangu ni huu, watu wote kwenye taifa wana haki ya kusema kupitia sanduku la kura nani wanayependa aongeze taifa.


Ni haki yao ya kisiasa , hivyo kama katiba inavyosema wana stahili zote na haki ya kuwa wagombea na wapigakura bila kujali kuwa wana ulemavu au watu wenye viungo vilivyokamilika.

Kwa hiyo wanastahili kuwa na mazingira na miundombinu wezeshi inayowafikisha kwenye kukamilisha mchakato wa kuamua viongozi wa kuwaongoza.




Wenye ulemavu wa kila aina wanahitaji kuwekewa mazingira ya kupiga a kura kwa siri kulingana na mahitaji yao. **PICHA: MTANDAO.**

# UCHAGUZI MAREKANI





Mgombea wa Democratic, Joe Biden (kushoto) na Rais Donalt Trump, wa Republican

**Na Mwandishi wetu**

## ■Trump azua hofu ya vurugu
## ■Akataa matokeo kabla ya kura

MAREKANI ni taifa ambalo linajipambanua kuwa kinara wa uchumi, nguvu ya kijeshi na baba wa demokrasia duniani.

Katika siku za hivi karibuni, taifa hilo limejikuta katikati ya mizozo ambayo inatishia kuharibu sifa za taifa hilo kubwa.

Baadhi ya mizozo iliyoibuka na kuyumbisha udhibiti wake, ni vitendo vya ubaguzi, janga la ugonjwa wa Corona na siasa zisizotabirika za Rais Donald Trump.

Kiongozi huyo anaelezwa ni mtu anayeweza kuidumbukiza nchi yake katika mgogoro mkubwa, kutokana na misimamo yake inayokwenda kinyume na matarajio ya wananchi wake wengi.

**“Nafikiria uchaguzi utaishia Mahakama ya Juu, nadhani ni muhimu tuwe na majaji tisa,” alisikika akisema Trump. Akaongeza “Nadhani ni vyema tukienda kwenye uchaguzi, kwa sababu nafikiria hii ni njama inayochezwa na Democrats, na njama hiyo itafikishwa mbele ya Mahakama ya Juu ya Marekani.”**

Wiki hii, Trump, ameibua wasiwasi mwingine baada ya kutoa kauli ambayo inaashiria kutokuwa na utayari wa kukabidhi madaraka endapo atashindwa katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Novemba.

Hata hivyo, ushindi wake wa nyuma ambao ulimwingiza madarakani, ulitawaliwa na utata kiasi ambacho Wamarekani wenyewe hawakutarajia kama atapata ushindi.

Rais Trump wakati akizungumza na Waandishi katika Ikulu ya White House, alisikika akisema suala la kukubali kushindwa halitakuwa jambo rahisi, anafikiria suala hilo litaamuliwa na mahakama.

“Tutaona kitakachofanyika, wote mnajua hilo.” Alisikika akisema baada ya kuulizwa kama yupo tayari kukabidhi madaraka kwa amani endapo atashindwa katika sanduku la kura.

Trump anapinga upigaji kura kwa kutumia posta, akifananisha sawa na janga na itaweza kuvuruga utaratibu wote wa uchaguzi.

Majimbo mengi yanatoa wito wa upigaji kura kwa kutumia posta, kutokana na hofu ya kuongezeka kwa visa vya corona endapo watu watapiga kura kwa njia ya kawaida.

“Napinga vikali upigaji kura kwa njia ya posta, upigaji kura wa namna hiyo ni majanga.” Alisema Trump.

Aidha akatoa wito wa uchaguzi huo kufutwa ili iwepo amani ndani ya nchi hiyo.

“Futeni uchaguzi na kutakuwa na amani, hapo hakutakuwa na suala la kupokezana madaraka, kwa kweli, kutakuwa na muendelezo.” Alisistiza.

Mwaka 2016, kiongozi hiyo alikataa kukubali matokeo ya uchaguzi katika kinyang'anyiro kati yake na mgombea wa Democratic , Hillary Clinton, hatua ambayo alitaja kama shambulio dhidi ya demokrasia ya Marekani.

Mwezi uliopita, Rais wa zamani wa nchi hiyo, Bill Clinton, alimtaka mgombea wa chama cha Democratic Joe Biden, kutokubali kushindwa katika mazingira yoyote.

Anaeleza kuna mpango wa Warepublican kuwatumia wapigaji kura feki na kisha kuwatumia kundi la mawakili kupinga matokeo ya uchaguzi.

Hata hivyo, wahafidhina wamemlaumu Biden kwa kuchochea vurugu katika uchaguzi kutokana na kauli yake ya mwezi Augosti, alipohoji kwamba kuna mtu anaamini hakutakuwa na vurugu nchini Marekani ikiwa Donald Trump atachaguliwa?”

**SAKATA LA JAJI**

Suala la uteuzi wa jaji mpya linaleta sintofahamu nyingine, baada ya Rais Trump kutetea uamuzi wake wa kumtafuta Jaji wa Mahakama ya Juu kabla ya uchaguzi.

Nafasi hiyo imeachwa wazi baada ya kifo cha jaji Ruth Bader Ginsburg, na hatua yake ya kuteua mtu mwingine anaifanya haraka akitarajia suala la matokeo ya uchaguzi lazima yatapelekwa mahakamani.

“Nafikiria uchaguzi utaishia Mahakama ya Juu, nadhani ni muhimu tuwe na majaji tisa,” alisikika akisema Trump.

Akaongeza “Nadhani ni vyema tukienda kwenye uchaguzi, kwa sababu nafikiria hii ni njama inayochezwa na Democrats, na njama hiyo itafikishwa mbele ya Mahakama ya Juu ya Marekani.”

Alifafanua kwamba leo atamteua jaji wa kike kuongoza mahakama hiyo ili kuziba nafasi ya Jaji Ginsburg, aliyefariki Ijumaa iliyopita.

Hata hivyo, wafuasi wa Trump, wanaamini uteuzi wake endapo utaidhinishwa na Bunge la Seneti, ataweka takwimu ya majaji 6-3 ya Wahafidhina kuongoza mahakama hiyo.

Kamishna wa Tume ya Uchaguzi, Ellen Weintraub, anapingana na kauli ya kiongozi hiyo, pale anaposema hakuna msingi wowote wa kufanyika kwa udanganyifu au njama ya kuiba kura.

Anasema kumekuwa na visa vichache vya udanganyifu katika mfumo wa upigaji kura kwa njia ya posta, akitolea mfano katika uchaguzi wa mchujo wa mwaka 2018, North Carolina, ambapo uchaguzi ulirudiwa tena baada ya kubainika mgombea wa Republican aliingilia mchakato wa upigaji kura.

Pia mwaka huu katika jimbo la New Jersey, madiwani wawili wa Democratic, walishitakiwa kwa kuhusika na udanganyifu uliohusisha upigaji kura kupitia posta.

Kiwango cha udanganyifu katika mchakato wa uchaguzi wa Marekani, uko chini kati ya asilimia 0.00004 na 0.0009, kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2017 uliofanywa na Kituo cha Haki cha Brenna.

**BBC,**

# Korea Kaskazini yaomba msamaha

**SOUL: Korea Kusini**

RAIS wa Korea Kaskazini Kim Jong-un, ameomba msamaha kufuatia mauaji ya ofisa mmoja wa Korea Kusini.

Kwa mujibu taarifa kutoka ofisi ya kiongozi huyo, Kim, alimwambia Rais wa Korea Kusini Moon Jae-in kuwa tukio hilo halikustahili kufanyika.

Korea Kusini inadai mtu huyo mwenye umri wa miaka 47, alikuwa akijaribu kutoroka kutoka Korea Kaskazini, baada ya kuonekana na wanajeshi wa nchi hiyo waliokuwa wakishika doria.

Katika tukio hilo, ofisa huyo alipigwa risasi, na kisha mwili wake ulichomwa moto.

Mpaka unaotenganisha nchi hizo mbili, unalindwa vikali, huku upande wa Kaskazini inaelezwa kutekeleza sera ya kuua kwa kumpiga risasi ili kumzuia asiingize virusi vya corona.

Maombi hayo ya msamaha yalitolewa kwa njia ya barua iliyotumwa kwa Rais Moon.

"Naomba msamaha kwa kuwakosea" Kim alimwambia Moon, kulingana na shirika la habari la Yonhap, likinukuu Ikulu ya Blue House.

Korea Kaskazini, ilikiri kumpiga risasi kumi mtu huyo na kwamba haikuchoma moto mwili wake, bali iliuweka katika kifaa kinachoelea baharini.

**DW**



Mtoto wa kiume akicheza na ng'ombe kwa kushika pembe zake kama alivyokutwa eneo la Dhi Qar, wilaya ya Chibayish, kilomita 120, Kusini Magharibi mwa mji wa Basra, nchini Iraq. **(PICHA: AFP)**

# Urusi yakamata mali za kiongozi wa upinzani

**BERLIN, Ujerumani**

URUSI inadaiwa kushikilia jengo na akaunti za kiongozi wa upinzani, Alexei Navalny, wakati akiwa hajitambui kutokana kile kinachelezwa kulishwa sumu.

Msemaji wa kiongozi hiyo, Kira Yarmysh, alimtuhumu tajiri mmoja mwenye uhusiano wa karibu na Ikulu ya Kremlin kuhusika na tukio hilo.

Alisema walikamata mali hizo wiki moja baada ya kuugua na kulazwa hospitalini akiwa hajitambui.

HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/alexei-navalny-atoka-hospitali-ya-berlin/a-55022812" Navalny ambaye ni mkosoaji mkubwa wa Rais wa Urusi, Vladimir Putin, aliruhusiwa kutoka katika hospitali alikokuwa amelazwa mjini Berlin mapema wiki hii, baada ya afya yake kutengemaa.

Kiongozi huyo wa upinzani alianguka na kupoteza fahamu Agosti 20, mwaka huu akiwa kwenye ndege inayofanya safari za ndani nchini humo.

Yarmysh kwenye taarifa yake aliyoitoa kwa njia ya video juzi, alisema kutokana na amri hiyo, jengo hilo haliwezi kuuzwa, kutolewa kama zawadi au kuwekwa rehani. Alisema pia akaunti za Navalny zilizuiwa kutokana na agizo la mahakama.

**DW**

# Ulaya yasema Lukashenko sio rais halali

**BRUSSELS, Ubeligiji**

UMOJA wa Ulaya (EU) umetoa kauli ya kuupinga utawala wa Rais Alexander Lukashenko, wa nchini Belarus.

Katika taarifa yake, Umoja huo ulisema hatua ya kuapishwa haraka Lukashenko, kuingia madarakani ni kitendo kilichokwenda kinyume na matakwa ya wananchi wa nchi hiyo.

Nchi zote 27 wanachama zimeweka saini taarifa hiyo ambayo inaona madaraka mapya ya kiongozi huyo yanakosa uhalali wa kidemokrasia.

Taarifa hiyo imekwenda mbali zaidi na kusema kuapishwa huko kwa Lukashenko, kunakwenda kinyume na matakwa ya Wabelarus kama ambavyo imejionesha kupitia maandamano.

**DW**

# Maelfu ya wahamiaji walirudishwa Libya

**NEWYORK, Marekani**

SHIRIKA la Kutetea Haki za Binadamu la Amnesty International, limesema maelfu ya wahamiaji waliokuwa wakikimbilia barani Ulaya walikamatwa na kurudishwa katika pwani ya Libya, waliachiwa huru na wapinzani wa serikali ya nchi hiyo.

Wahamiaji hao waliondolewa kwa nguvu katika vituo visivyo rasmi vya kuwaweka wakimbizi vinavyoendeshwa na wanamgambo wanaoshirikiana na serikali ya Libya inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa.

Ripoti mpya ya shirika hilo ilieleza vikosi vya wanajeshi vinavyopambana na serikali ya Libya, iliwaondoa kwa nguvu maelfu ya wahamiaji bila ya kufuata utaratibu au kuwapa nafasi wakimbizi hao kurudishwa walikotoka.

Amnesty ilisema kiasi wahamiaji 8500 wakiwamo watoto na wanawake, walikamatwa na kurudishwa nchini Libya, kati ya mwezi Januari na Septemba.

**DW.**

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

## VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa eneo la Mkundi/Banana mtaa wa bwawani -Morogoro. Ina vyumba vinne self container, sebule, dining room na choo cha nje ndani ya fensi. Wasiliana na simu 0713-435172/0713-440436.

## VIWANJA/MASHAMBA

**ENEO LINAUZWA,** Eneo linauzwa Makongo juu Dar-es-salaam karibu na Petrol Station mwisho wa lami Lina Nyumba nne za kuishi, umeme, maji ya kisima na dawasco ipo ndani ya fensi. Wasiliana na simu: 0753-029141/0779-999041.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Hassan Hamisi Konza** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **PREMIO** yenye namba ya usajili **T734 DJR** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa:

**KUMB.NA.DO.B.I/21/VOL.IX/757**

115917302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUSSEIN RAMADHAN MKUMBI**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T270 CD116**

CHASSES NO **EP3WF100611**

ENGINE NO **L33472924**

RANGI METALIC SILIVER

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**ARU/ARU/RB/683383/2020.**

115917002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;281/2020**

**Ombi la CAROLYNE KIBUA ITEBA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHARLES WILLIAM ITEBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 21/09/2020.

Tarehe 21/9/2020

Sahihi ya Hakimu

115917202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;281/2020**

**Ombi la HUSSEIN MOHAMED KIMARO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MOHAMED SAID KIMARO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/09/2020.

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU

115917102

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA. 14 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SALUM BAKARI URASSA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**ISSA BARAKA URASSA**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 9 mwezi wa October 2020
Imewasilishwa Dar es Salaam. Leo tarehe 9 mwezi wa September 2020

.....................................
**NAIBU MSAJILI**

**NAKALA KWA:**
**NIPASHE**
**NEWS PAPERS**

NAIBU MSAJILI

115916502

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
Tarehe 25/09/2020

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 26/09/2020** kampuni ya **ALFREDY CHARLES NJUJU** itasafirisha Mzigo wake yenye vipimo vikubwa. Kutoka **SONGEA (KITAI) kuelekea MUSOMA** kupitia **MOROGORO** Magari hayo yenye namba za usajili namba za usajili:
   **1. T598 DNS/T656 BYF**
   **2. T834 DGB/T898 DCY**
   **3. T462 AWG/T588 AXB**
2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **22** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **4.75** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **5.20** |

3. Gari hizo zinatoka **SONGEA(KITAI) kuelekea MUSOMA kupitia MOROGORO.** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115916902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Global Publishers General Enterprises Ltd** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba **T755 CNT** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa:

**DAR/KIJ/RB/689451/2020**

115916401

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWIGO HOLDING LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 703 DGF** rangi nyeupe,Chassis namba **TRH2000028237** Engine namba **ITR0220574** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi

**MBE/KYE/RB/670187/2020**

115917902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:...272..2019**

**Mdai: MOHAMEDI ATHUMANI**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: MATHIAS JOHN KABELEBENZE**

**Kwa: MATHIAS JOHN**
**KK.MTAA**
**K/MBUYUNI**

**Ombi la Mdai: MOHAMEDI ATHUMANI**
**Madai ya: PESA TSH.3,720,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 16 mwezi 10 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo **tarehe 23 mwezi 09 mwaka 2020.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115917902


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie

0782253676


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-31

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.
Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.
Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

Pamoja yote, bado akili ya kikachero iliendelea kumwambia awe na tahadhari, kwani watu wanaoitafuta roho ya Shani bado wapo na wanafanya kazi mchana kutwa kuhakikisha msichana huyo haendelei kuwa duniani.

Ingekuwa rahisi tu kama angemwambia Shani kuwa kuna watu wanamtafuta ili wamuue, lakini alikuwa hataki kabisa kumwambia hilo.

"Ina maana Sherry, mimi kukwambia tukae wote nyumbani ni kosa?"

"Hapana nauliza tu."

"Basi kwa sasa ningependa kuwa karibu zaidi na wewe."

"Mhhh jamani, haya, mimi nimekubali."

"Sawa lakini kwa muda kwanza."

"Hata moja kwa moja siyo mbaya, mimi ni wako tu."

"Hapana, baadaye nataka urudi nyumbani kwako, ili nifanye taratibu zinazotakiwa."

"Taratibu gani?"

"Si za kuoa."

Jibu hilo lilimtia ganzi Shani. Hakutegemea neno hilo kwa sasa kutoka kwa Eddy. Alivuta picha atakavyokuwa mke halali wa mwanaume huyo aliyetokea kumhusudu mno. Mtu aliyebadilisha maisha yake na kuwa na furaha na amani muda wote.

"Kweli utanioa Eddy?"

"Kama nisipokuoa wewe nikamuoe mwanamke gani mwingine. Si bora tu basi nikae bila kuona."

Majibu hayo yalimfanya Shani abubujikwe na machozi. Akamkumbatia Eddy. Alijihisi kama tayari amekuwa mke wake.

Ni kweli kabisa Eddy alikuwa amempenda kwa dhati Shani. Akili ya kumuoa ilikuwepo. Wakati Shani akidhani itakuwa ni kazi rahisi tu, mwenzake aliwaza kwanza jinsi ya kumaliza tatizo zito linalomzunguka Shani.

Tayari alikuwa amezima jaribio la kumuwekea sumu kwenye chakula. Lakini kabla ya kumuoa, alijua kuwa tukio zito linaandaliwa kwa ajili ya msichana yule kama watesi wake wakigundua kuwa yuko hai baada ya miezi mitatu kupita. Ni lazima waandae mpango mwingine wa kumuangaliza. Mpango gani? Wa sumu? Risasi? Kumtengenezea ajali? au kumteka. Wakati Eddy akiwa amekumbatiwa na Shani, akili yake iliwaza mengi.

"Ni lazima niwasake hawa watu kabla hawajafanya chochote juu ya mrembo huyu." Alijiambia.




*******************************

"Usiponiambia ukweli nitakuua."

"Basi, basi kaka nitakwambia, niache unaniumiza."

Ilikuwa ni sauti ya kilio iliyotoka kwa kijana aliyekadiriwa kuwa na miaka isyopungua 25.

Ilikuwa ikilia na kuomboleza kutokana na maumivu makali ya mateso aliyokuwa akiyapata.

Kiasi cha dakika 10 tu, tayari kijana huyo alikuwa hoi.

"Sema. Ukisema nitakuachia, lakini ukijifanya kunificha, basi humu leo hutotoka ukiwa hai."

"Ni kweli kaka mimi ndiye niliyemuua Fikiri."

"Okay, sasa niambie ulimuua kwa kutumia nini?" Mtesaji aliendelea kuhoji.

"Nilimuua kwa kumpiga gongo kichwani." Alijibu huku akigugumia kwa maumivu.

"Ulimpiga wapi na mangapi?"

"Matatu kichwani kaka, ila nisamehe, usiniue lakini."

"Ukijibu maswali yangu vizuri sikuui, ila ukijifanya unajua, basi utamfuata Fikiri uliyemuua."

"Nisamehe kaka yangu, njaa tu hizi."

"Njaa ndiyo unaua mtu? Wewe si kijana mwenye nguvu zako kabisa, kwa nini uliua mtu?"

"Nilipewa shilingi laki moja ili niue."

"Nani aliyekutuma?"

"Simjui."

Ni jibu lililoonekana kumkasirisha mtesaji.

"Inakuwaje unaua mtu unayemfahamu kwa kutumwa na mtu usiyemfahamu?"

"Dah, we acha tu kaka yangu, shetani tu alinipitia."

"Mimi nitajuje kama unasema kweli au uongo, inawezekana unamjua."

Kijana alianza kulia, akijua kabisa mateso yataendelea.

"Nataka uniambie, huyu mtu jinsi alivyokuja mpaka akakuchagua wewe ukamuue Fikiri na kama alikwambia sababu za yeye kukutuma."

"Kaka mimi pale mitaa ya Kigogo ndiyo wananitegemea, yaani ndiye mtemi wao, sasa alikuja mtu na gari yake pale, akata mtu ili akamfanyie kazi yake, akaambiwa kuwa mimi naweza, nikaingia kwenye gari yake, akanichukua mpaka njia panda ya Kigogo, Magomeni na Msimbazi Kota, akapaki gari na tukakaa ndani akanipa maelekezo ya kufanya," alisema akasita kidogo.

"Kusema kweli kaka, inavyoonekana tayari alikuwa ameshapeleleza na kufahamu mienendo yote ya Fikiri, akaniambia anatembea na mkewe, kwa hiyo anataka afe, ndiyo hivyo tu, akanipa hiyo pesa, mimi nikamvizia anatoka ulevini nikamuua."

"Huyo mtu yukoje?"

"Mrefu mwembamba mweusi hivi. Hajaniambia jina, wala anakotoka, lakini si mtu wa maeneo ya Kigogo kwa sababu hata mimi ni mara ya kwanza kumuona."

Alionekana kuamini maneno ya kijana yule. Kwa sababu aliyoyatoa yote yaliyonekana yalikuwa sawa. Aliamua kusema ukweli kwa ajili ya kujiokoa, hivyo angemjua angesema tu.

"Hata namba ya gari yake huijui?"

Aliogeuza kichwa, akaangalia juu kisha akasema "Mh, namba? Nadhani ni namba 500."

"Unadhani au una uhakika?"

"Huo uhakika, gari yake imesajiliwa namba 500."

"Mbona hii kaka umeijua kwa haraka zaidi?"

"Niliposhuka, wakati ananipa hiyo pesa na kuondoka niliiona hiyo namba, halafu hata alipokuja usiku kwa ajili ya kuangalia kama kazi yake inafanyika, alikuja nalo na namba ya gari ndiyo ilinifanya nijue kama ni yeye alipofika pale tulipoahidia tukutane."

Jibu hilo lilimfanya Eddy kumaliza maswali kwa kijana huyo. Aliridhika na baadhi ya maswali, likiwemo hilo la mwisho.

Alichofanya ni kupiga simu, na mmoja wa wasaidizi wake alifika. "Nenda na huyu, kamkabidhi kwenye ofisi za Makao Makuu ya Polisi mpaka hapo nitakapotoa taarifa nyingine, sawa."

Msaidizi wake aliitikia na kuondoka na mtuhumiwa.

Jina lake halisi aliitwa Faustin. Huyu ndiye aliyekiri mwenyewe kuwa alimuua Fikiri. Alipatikana na Eddy kirahisi tu.

Eddy alikwenda maeneo ya Kigogo kuulizia alipokuwa akiishi marehemu Fikiri kwa ajili ya kuangalia kama angepata chochote kitakachoweza kumfanya agundue kitu.

Alipouliza alipelekwa moja kwa moja hadi alipokuwa akiishi na kukutana na mkewe na familia yake.

Alijitambulisha kama mmoja wa wateja wake kule ABC ambaye alikuwa amesafiri nje ya nchi, hivyo alivyorudi alikuta taarifa ya kifo cha rafiki yake huyo, hivyo ameamua kwenda kutoa mkono wa pole na rambirambi.

Wakati akiwa huko, aliwasikia baadhi ya vijana wakimshangaa mwenzao mmoja anayeitwa Faustin kuwa kwa muda wa wiki nzima amekuwa akitamba kwa kununulia watu pombe.

Akamsikia mmoja akisema wanamfahamu Faustine, mara nyingi kazi yake ni kukodiwa na watu wanaotaka kuwadhuru wengine, kwa kuwapiga au kuwafanyia vitu vibaya na wengine wao ni wale ambao wanawahisi wanatembea na wake zao, au hukodiwa na wanaume wanapotaka kwenda kuwafumania wake zao.

Hii ilimfanya kumuulizia mtu huyo, na yeye akijifanya ana tatizo hilo. Aliletewa, lakini mapatano yalikuwa ni Sh 300,000 kwenda kwenye fumanizi.

Aliingia kwenye gari la Eddy. Badala ya kwenda alikodhani, alipelekwa kwenye ofisi ndogo ya Eddy ambayo mara nyingi hutumika kuwafanyia usaili au kuwalazimisha wale wote anaotaka waseme anachotaka, au anachodhani kuwa wanaficha kukisema.

Hivi ndivyo Faustine alivyoingia kuilaini kwenye mikono ya Eddy.

***Itaendelea Jumamosi***




# UNITED

## KUTOA OFA YA MWISHO KWA SANCHO

**DORTMUND, Ujerumani**

MANCHESTER United itatoa ofa ya mwisho ya ama "kataa au kubali" kwa nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, kwa mujibu wa magazeti ya Daily Star na Mirror.


Thamani ya Sancho inaonekana kuwa kikwazo kwa United, ambao wanamuwania kwa udi na uvumba kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa England.

Ingawa United inaonekana kukata tamaa, lakini sasa imeripotiwa kwamba itajaribu kutoa ofa ya mwisho kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka pale katika dimba la Old Trafford, Man United sasa watatoa ofa hiyo ya mwisho ya "kataa au kubali" hapa ndio mwisho.

United haijawa tayari kutoa kiasi cha euro milioni 120 kinachotakiwa na Dortmund ili kumuuza Sancho.

Kwani wao Man United wapo tayari kutoa kiasi cha euro milioni 98 na si zaidi ya hapo.



## Rais wa Lyon aitaja Arsenal kwa Aouar

**LYON, Ufaransa**

RAIS wa Klabu ya Lyon, Jean-Michel Aulas, ameitaja Arsenal wakati akijadili kuhusu majaliwa ya kiungo wao, Houssem Aouar.

Aouar amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England, Arsenal, pamoja na Manchester City, Paris Saint-Germain na Chelsea baada ya Lyon kumaliza msimu wa 2019-20 kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lyon imemthaminisha Aouar kwa euro milioni 60 na inakataa kushuka bei hiyo huku kocha Mikel Arteta akipambana kutafuta fedha za kutaka kumsajili pale Arsenal.

Alipoulizwa kama Aouar anaweza kubakia kwa klabu hiyo ya Ligue 1, Aulas aliiambia Le Progres: "Kifedha, Arsenal ni kama timu yoyote ambayo imeathirika na mlipuko wa virusi vya corona.

"Na Houssem anaweza kujisemea mwenyewe kwamba jambo bora litakuwa ni kubakia na sisi."

Nahodha wa Lyon, Memphis Depay, pia amekuwa akihusishwa na Barcelona na AC Milan, wakati Moussa Dembele akiendelea kuwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya.

# Bale anastahili heshima Real Madrid - Ramos

**MADRID, Hispania**

GARETH Bale ameipa kila kitu Real Madrid na anabakia kama "nyota mwenye kipaji cha daraja la juu", kwa mujibu wa kocha wake wa zamani, Juande Ramos.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales alikamilisha usajili wa mkopo kurudi Tottenham wiki iliyopita, miaka saba baada ya kuondoka pale kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia wakati huo.

Ameshinda mataji 13 wakati akicheza pale Santiago Bernabeu, yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini alikumbwa na wakati mgumu kwa misimu kadhaa iliyopita.


Madrid hawakuonyesha kujali sana kuondoka kwa Bale na Ramos amebainisha kwamba, nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, anastahili heshima zaidi.

"Ni mchezaji ninayempenda sana," alisema Ramos, ambaye aliimnoa mshambuliaji huyo wakati akiwa pale Tottenham na pia aliimnoa kwa kipindi cha miezi sita wakati akiwa kule Madrid, akiiambia redio Marca.

"Nafikiri ameipa Real Madrid mengi sana. Alikuwa na nguvu kubwa kwa mguu wake wa kushoto. Ni mchezaji aliyetumika sana na ni mmoja wa nyota wenye vipaji vya daraja la juu."

Bale alifunga mabao 105 na kuchangia 57 katika mechi 251 kwa Madrid, lakini msimu uliopita hakupata nafasi kubwa ya kucheza baada ya kuwa na uhusiano mbaya na kocha, Zinedine Zidane.

"Ndani ya Madrid pengine wanajua matatizo aliyokuwa nayo na Zidane," alisema Ramo. "Lakini ana habari yake binafsi kwa mafanikio pale."





# KLOPP

## AFURAHIA USHINDI, LIVERPOOL KUIVAA ARSENAL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekielezea kikosi chake kama kilikuwa "rahisi machoni" wakati wakiibuka na ushindi wa 7-2 dhidi ya Lincoln City kwenye mchezo wa Kombe la EFL, Alhamisi.

Curtis Jones na Takumi Minamino kila mmoja alifunga mara mbili, wakati Xherdan Shaqiri, Marko Grujic na Divock Origi pia walifunga kwenye mchezo huo na sasa watakabiliana na Arsenal kwenye raundi ya nne wiki ijayo.

Klopp, ambaye alifanya mabadiliko 10 katika kikosi hicho kutoka kile kilichoifunga Chelsea kwenye Ligi Kuu wikiendi iliyopita na kumuanzisha Diogo Jota katika mchezo wake wa kwanza kipindi cha pili, alifurahishwa na kiwango cha wachezaji wake.

"Tulicheza soka zuri usiku huu," alisema akiiambia BBC Radio 5 Live. "Ilikuwa timu rahisi kwenye macho.

"Tulipasiana vizuri mpira. Vijana walitaka kucheza soka na walionyesha ari ya aina yake.

"Hivyo ndivyo tulivyotakiwa kuwa. Ukivaa jezi ya Liverpool lazima uwe mchezaji mwenye ari kubwa uwanjani. Nina furaha na kila kitu.

"Mabao mawili tuliyoruhusu hayakuwa mazuri, lakini si tatizo kubwa. Unaweza pia kuwa kwenye wakati mgumu katika mchezo kama ule."

## MULLER AMVULIA KOFIA MARTINEZ

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller amemsifia nyota mwenzake wa Bayern Munich, Javi Martinez kwa kufunga bao la ushindi dhidi ya Sevilla.

Martinez alifunga bao la ushindi Alhamisi usiku na kuwawezesha Bayern kutwaa taji la Super Cup, baada ya kuibuka na ushindi wa 2-1 katika muda wa ziada.

Mchezo huo uliowakutanisha bingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na yule wa Ligi ya Europa ulimalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1 katika muda wa kawaida, kwa mabao ya Leon Goretzka aliyeifungia Bayern na Lucas Ocampos kwa Sevilla.

Ilikuwa ni mara ya pili kwa kiungo huyo kufunga bao la ushindi kwa muda wa ziada akitokea benchi, kwani pia alifunga katika dakika ya 121 dhidi ya Chelsea mwaka 2013 wakati Bayern walipotwaa taji hilo.

Muller aliiambia UEFA.com: "Tumefurahi, hatukuamini. Tulikuwa tumechoka sana baada ya dakika ya 120 dhidi ya Sevilla.

"Tulipambana sana na tulionyesha kuwa sisi ni timu ambayo ilikuwa na ari kubwa ya ushindi, hata kama hatukuwa kwenye ubora wetu.

"Hongera kwa timu na Javi Martinez."

# Juventus ina furaha chini ya Pirlo - Ramsey

**TURIN, Italia**

JUVENTUS wana "furahia zaidi" chini ya kocha mpya, Andrea Pirlo ikilinganishwa na msimu uliopita wakati Maurizio Sarri alipokuwa kocha, kwa mujibu wa kiungo Aaron Ramsey.

Pirlo alitajwa kuwa mrithi wa Sarri mwezi uliopita na alianza kuiongoza kwenye mchezo wake wa kwanza wa kiushindani wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Sampdoria wiki iliyopita. Ramsey, ambaye hakuwa na nafasi nyingi ya kucheza msimu uliopita, alitengeneza pasi za mwisho sita, ikiwamo dhidi ya Cristiano Ronaldo.

Na mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales amebainisha namna gani hali ilivyobadilika kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya kuteuliwa kwa kiungo huyo wa zamani, Pirlo kuinoa.

"Tuna kocha mpya, watu wapya, mawazo mapya na wachezaji wako poa kabisa," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Nafikiri tuna furaha zaidi kuliko mwaka jana. Mazoezi ni magumu lakini pia kuna hali kubwa ya kufurahia."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG AMSHUKURU AERTA KUMBAKIZA ARSENAL

**Kwa uhakika kabisa najivunia kuwa nahodha, lakini si sababu kubwa ya kubaki kwani...**

**LONDON, England**

PIERRE-Emerick Aubameyang alikuwa na nafasi nzuri ya kuondoka Arsenal, lakini amemtaja kocha, Mikel Arteta, kama sababu kubwa ya yeye kuchagua kubakia hapo kwenye dimba la Emirates.

Aubameyang alisaini mkataba wa miaka mitatu kubaki na klabu hiyo ya London Kaskazini na kumaliza uvumi wa kwamba anaondoka.

Barcelona na Inter Milan zilikuwa miongoni mwa klabu kubwa za Ulaya zilizohusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye amedai alikuwa akitaka changamoto mpya.

"Nilikuwa nafikiria kuhusu hilo kuwaambia ukweli kwa sababu nilikuwa tayari na nafasi nzuri ya kuondoka," alisema akiiambia Sky Sports.

"Lakini najisikia vizuri kuwa hapa - mapenzi kutoka kwa mashabiki na klabu nzima - sina uhakika kama kwa kuondoka ningepata mapenzi sawa, ndio maana nimeamua kubaki.

"Kwa uhakika kabisa najivunia kuwa nahodha, lakini si sababu kubwa ya kubaki. Bila shaka ni kazi kubwa kuifanya, lakini haikuwa sehemu ya mimi kubaki hapa."

Alikuwa ni Arteta - ambaye mara kwa mara alikuwa akielezea kuwa na imani kwamba, Aubameyang atasaini mkataba mpya na amekuwa na ushawishi mkubwa kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon.

"Tangu amekuja hapa, ameleta vitu vingi sana chanya na falsafa mpya kwa upande wetu," alisema Aubameyang.

"Nafikiri hilo lilikuwa muhimu kwa sababu likanifanya kiwango changu kuwa juu na kujihisi kwamba nahitaji kuimarika zaidi. Nafikiri hii ilikuwa sababu kubwa zaidi."

Aubameyang aliongeza: "Tulikuwa tunawasiliana wakati tukiwa 'lockdown' na tulikuwa tunazungumza kuhusu mechi na alisema, 'sawa, sahau kuhusu hilo, tutazungumza baadaye' na aliniuliza nini nataka kufanya.

"Nikamwambia najisikia vizuri, naimarika na falsafa mpya ni mzuri sana na hivyo nataka kubaki hapa na ananiambia nitaacha kumbukumbu nzuri zaidi."

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMTAKA JORGINHO**
ARSENAL imeonyesha nia yao ya kutaka kumsajili kiungo wa Chelsea na Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports - via Mail)***

**CITY WAIGOMEA ATLETICO**
MANCHESTER City imedai kwamba ofa ya pauni milioni 78 kwa mlinzi wa Atletico Madrid na Uruguay, Jose Gimenez mwenye umri wa miaka 25, ni kubwa mno. ***(Goal)***

**PERTEY HUYOOO ARSENAL**
KLABU ya Atletico Madrid inaamini itamsajili Lucas Torreira kwa mkopo, katika dili ambalo Arsenal itamsajili kiungo, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27 raia wa Ghana. ***(Sky Sports)***

**UTD YAKATAA BEI YA TELLES**
BEI ya Alex Telles iliyotajwa na FC Porto ya pauni milioni 18.3 inaonekana kuwa kubwa mno kwa Manchester United kwa sababu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, atakuwa huru msimu ujao. ***(Guardian)***

**TORREIRA KUONDOKA ARSENAL**
LUCAS Torreira anajiandaa kuondoka Arsenal, huku Atletico Madrid na Torino zikionyesha nia ya kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 24. ***(Independent)***

**PSG YAACHANA NA DELE**
KLABU ya Paris St-Germain ina matumaini kujitoa kwenye mazunguzo ya kumsajili Dele Alli kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Telegraph)***

**HUDSON-ODOI KUONDOKA CHELSEA**
STRAIKA wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19, anataka kuondoka pale Stamford Bridge kwa mkopo. ***(Talksport)***

**COUTINHO KWENDA ARSENAL**
KIUNGO wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28, anaweza kwenda Arsenal kwa mkopo kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Star)***

**MILIK AWANIWA EVERTON**
STRAIKA wa Napoli, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26, amehusishwa na mpango wa kujiunga na Everton inayonolewa na kocha, Carlo Ancelotti. ***(Star)***

**MONACO YAMUWANIA DELE**
MONACO imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Tottenham na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, ***(90min).***

**BREWSTER AWINDWA SHEFFIELD**
KLABU ya Sheffield United inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili straika wa Liverpool, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 20, huku Aston Villa, Brighton na Crystal Palace pia zikionesha nia kutaka kumsajili. ***(Independent)***



HABARI MICHEZO

# YANGA TAYARI KWA MTIBWA, MCHAKATO LA LIGA WAIVA

**Somoe Ng'itu, MOROGORO**

**na Saada Akida, DAR**

WAKATI kikosi cha Yanga kutoka jijini Dar es Salaam kiliwasili salama mkoani hapa jana mchana tayari kwa mchezo wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Mtibwa Sugar utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri, uongozi wa klabu hiyo umesema ripoti ya mwisho ya makubaliano ya kimfumo kutoka La Liga kupitia Klabu ya Sevilla sasa umeiva.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia Nipashe kuwa wamefika salama na wanatarajia kuendelea na maandalizi ya mechi hiyo wakiwa na wachezaji wao wote.

Hafidh alisema kila mchezaji yuko tayari kuikabili Mtibwa Sugar na wanajua wapinzani wao wamejipanga kutopoteza pointi kwa mara nyingine.

"Tumeshafika Morogoro, tunajua upinzani utakuwapo, Mtibwa Sugar si timu ndogo, tumewaangalia mechi zao zilizopita na kujua uwezo wa kila mchezaji, hatutazubaa, tutaongeza umakini wakati wote wa mchezo," alisema meneja huyo.

Naye Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema timu yake imeimarika na iko tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita na amewataka Yanga wajiandae kupokea 'kichapo' hapo kesho.

Kifaru alisema ushindi walioupata katika mechi iliyopita dhidi ya Ihefu FC umewapa nguvu na wanaamini kasi yao haitarudi nyuma kwa sababu hawataki kujiweka tena kwenye 'presha' ya kujinusuru kushuka daraja.

"Msimu huu tuko vizuri sana, hatutaomba tena Watanzania watuombee dua, tumesajili wachezaji wenye uwezo na wanaopambana kusaka ushindi, wasitarajie mteremko, tunawaambia watapoteana," Kifaru alisema.

Wakati hayo yakijiri mjini Morogoro, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said, amesema wiki ya mwanzo ya mwezi ujao wanatarajia kupokea ripoti ya mwisho ya makubaliano ya kimfumo ya timu hiyo kutoka Kampuni La Liga kupitia Klabu ya Sevilla.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Hersi alisema mchakato huo umefika hatua nzuri na ripoti hiyo ni ya mwisho kutoka La Liga kushirikiana na klabu hiyo ambayo wanatarajia kukabidhiwa wiki ya mwanzo ya mwezi ujao (Oktoba), mwaka huu.

Alisema baada ya hatua ya kwanza ya makabidhiano, watapata utaalamu wa ndani, na kisha watautoa nje kwa kushirikisha matawi yote ya Yanga nchini nzima.

"Baada ya kupata utaalamu huo katika matawi yote ya Yanga kuelimisha na kupata ushauri wa wanachama kutokana na ripoti hiyo baadaye itapelekewa katika mkutano mkuu kupata ridhaa ya wanachama wote.

"Niwaombe mashabiki na wanachama wa Yanga, kuunga mabadiliko hayo ya kimfumo kwa sababu baada ya kukabidhiwa ripoti hiyo tutawashikirisha wanchama wetu kabla ya kupeleka katika mkutano mkuu," alisema Hersi.

Alisema pia mashabiki wajitokeze kwa wingi kusapoti timu yao ikiwa ni pamoja na kununua jezi halali na kujitokeza kwa wingi katika viwanja inapocheza timu yao.

TUPO TAYARI...



Kiungo Mzimbabwe wa Azam FC, Never Tigere, baada ya kuwasili mjini Sumbawanga, Rukwa juzi, tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji, wahamiaji Tanzania Prisons ya Mbeya itakayopigwa leo katika Uwanja wa Nelson Mandela. **MPIGAPICHA WETU**

# Biashara yaongeza 'silaha' kuivaa JKT Tanzania

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema amefanya ongezeko la wachezaji katika kikosi chake kwa kuleta viungo wake wawili waliobakia Musoma mkoani Mara kuja kuongeza nguvu katika mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Baraza alisema viungo hao ni Juma Mpakala na Bernard Manumbo ambao hawakuwapo katika mechi iliyopita dhidi ya Simba kutokana na kuwa majeruhi.

Alisema nyota hao walibaki Musoma na juzi wamejiunga na wenzao kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao kuelekea mechi yao hiyo ambayo wanahitaji pointi tatu.

"Wachezaji hao walibaki Mara kwa sababu ya kuwa majeruhi na walikuwa na program maalum, sasa wamejiunga kikosini kuimarisha safu ya kiungo ambayo ilikuwa ina upungufu na kusababisha mechi dhidi ya Simba kufungwa mabao mengi huku tukishindwa kufika mbele," alisema Baraza.

Alisema kuelekea mechi yao hiyo wamejiandaa vizuri na wapo tayari kutafuta pointi tatu katika mechi hiyo ambayo wanacheza ugenini.

Kocha huyo alisema wana waheshimu wapinzani wao ila wamejipanga kupambana kutafuta matokeo chanya katika mechi hiyo.

Biashara itakuwa mechi yao ya nne baada ya kushinda mechi mbili za nyumbani na kufungwa bao 4-0 dhidi ya Simba wiki iliyopita katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam.

## Malindi kusajili wapya wanne

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Malindi imetangaza kusajili wachezaji wanne watakaoziba pengo la nyota wake tegemeo walioondoka klabuni hapo katika dirisha hili la usajili.

Wachezaji hao walioachana na 'Wekundu wa Mjikongwe' msimu huu ni mlinda mlango namba moja Ahmed Ali Salula, Ali Juma Maarifa "Mabata", Abubakari Ame na Ibrahima Baka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa timu hiyo, Kau Howingkao, alisema kwa sasa kocha ana kazi ya kusaka wachezaji ambao wataziba pengo la nyota walioondoka katika timu hiyo kwenda kutafuta malisho kwingineko.

Alisema kwa hatua ya awali, tayari wapo katika mazungumzo na wachezaji wanne ambao hata hivyo hakuwa tayari kuwataja majina kwa sasa, lakini akisema wametokea katika timu za Ligi Kuu Zanzibar.

Hata hivyo, timu hiyo imesema kwa msimu huu itakuwa chini ya Kocha mpya, Mohmed Hafidh Badru.

## Tanzanite yaimarika ikiiwinda Senegal

**Na Adam Nyangasa, TUDARCo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 20 (Tanzanite), Bakari Shime, amesema tayari kikosi hicho kimeanza maandalizi ya awali ili kutengeneza muunganiko mzuri, kuelekea mechi ya mtoano ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Senegal.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema, maandalizi hayo yameanza mapema kwa sababu timu hiyo haikuwa pamoja kwa kipindi kifupi, lakini mpaka sasa wachezaji wote wako vizuri na salama na wanaendelea na mazoezi.

**"Niseme tu ndani ya hizi siku tatu za maandalizi, timu imeshaanza kurudi katika hali yake na ninaamini kwa hizi juhudi ambazo Shirikisho la Soka nchini (TFF) limeweka, tutahakikisha tunarudi katika kiwango chetu, tunaweka umakini na nguvu zetu hapa ili kuhakikisha tunafika Kombe la Dunia," alisema Shime.**

Alisema, TFF limewekeza pesa nyingi kuiweka timu hiyo katika maandalizi mazuri, kwa kuhakikisha inakaa kambini, inacheza michezo mingi ya kirafiki ili kujiweka katika sehemu nzuri kuweza kusonga mbele na kufuzu michuano hiyo itakayofanyika mwakani.

Michezo
Jumamosi Septemba 26, 2020
Nipashe



AUBAMEYANG AMSHUKURU AERTA KUMBAKIZA ARSENAL HABARI UK 22

KWA WATURUKI...




Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akisaini mkataba wa kujiunga na Klabu ya Fenerbahce ya Uturuki kwa mkopo wa mwaka mmoja, jana mbele ya viongozi wa klabu hiyo, akitokea Klabu ya Aston Villa ya England. **PICHA: MTANDAO**

## SAMATTA AFUNGUKA AKITUA FENERBAHCE

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, amejiunga rasmi na Fenerbahce ya Uturuki kwa mkopo wa mwaka mmoja kutoka Aston Villa ya England.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Aston Villa, Samatta mwenye umri wa miaka 27, ametua klabu hiyo ya Uturuki kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu na baada ya msimu huo atauzwa moja kwa moja kwa ada ya pauni milioni 5.5 (Sh. bilioni 16.17 za Tanzania) ambayo inaweza kuongezeka hadi kufikia pauni milioni 6.2 (sawa na Sh. Bilioni 18.2 za Tanzania.

"Nafahamu Fenerbahce ni klabu kubwa kiasi gani," Samatta alisema.

"Ni mwenye furaha kuwa hapa katika familia hii kwa sababu itakuwa mpya na changamoto kubwa kwangu.

"Fenerbahce ina mashabiki wengi na mara zote wanataka kushinda. Na mimi pia nataka kushinda. Nimekuja kwa ombi hili, ninafuraha sana na ninatumai tutashinda mataji mengi."

Taratibu zote za mkataba huo zinaweza kukamilika na Samatta kuwahi mchezo dhidi ya mahasimu wa Fenerbahce, Galatasaray kesho Jumapili.

Samatta alijiunga na Aston Villa Januari mwaka huu kwa dau la pauni milioni 10 kutoka Klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji akisaini mkataba wa miaka minne na nusu.

Amecheza mech 14 tu hadi sasa na kufunga mabao mawili – Aston Villa ikichapwa 2-1 na wenyeji, AFC Bournemouth mechi ya Ligi Kuu alifunga kwa kichwa dakika ya 70 Uwanja wa Vitality.

Samatta alifunga tena bao la kufutia machozi Aston Villa ikichapwa 2-1 na Manchester City katika fainali ya Kombe la Ligi (EFL Cup) kwenye Uwanja wa Wembley jijini London.

# SIMBA, AZAM VITA YA KILELENI LIGI KUU LEO

## ●●●Ni baada ya KMC FC kupanguliwa gia Kagera, Kocha Sven, Gwambina FC watoa neno...

**Na Somoe Ng'itu**

VITA ya kuwania kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa mabingwa watetezi ligi hiyo, Simba kuikaribisha timu mpya ya Gwambina FC kutoka Misungwi, Mwanza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Mechi nyingine ambazo zitaamua nani akae kileleni leo ni ile ya Azam FC dhidi ya wenyeji Tanzania Prisons waliohamia Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa pamoja na mchezo kati ya Dodoma Jiji yenyewe ikiwa mgeni wa Polisi Tanzania katika dimba la Ushirika mjini Moshi.

KMC ambayo ipo kileleni hadi sasa kwa tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa, ikiwa na pointi tisa sawa na Azam FC baada timu hizo kushinda mechi zake tatu za mwanzo, jana ilipoteza mchezo wake wa raundi ya nne kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

Bao hilo lilifungwa na Yusuph Mhilu akiitendea haki krosi ya David Brayson katika kipindi cha kwanza hivyo kuifanya KMC hatima yake ya kukaa kileleni kusubiri matokeo ya mechi za leo.

Hivyo, endapo Azam itashinda leo itafikisha pointi 12 na kukaa kileleni kwa kuishusha KMC ambayo inaweza kuporomoka hadi nafasi ya nne endapo Simba na Dodoma Jiji zenye pointi saba kila moja, itashinda mechi yake leo.

Azam itashuka dimbani ikitoka kushinda bao 1-0 kwa mbinde ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine dhidi ya Mbeya City, wakati Dodoma Jiji yenyewe ikitoka kulazimisha sare tasa katika Uwanja wa Mkwakwani dhidi ya Coastal Union.

Simba itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 4-0 walioupata dhidi ya Biashara United wakati Gwambina FC yenye pointi moja walifungwa goli 1-0 na Ruvu Shooting.

Akizungumza na gazeti hili kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, alisema kikosi chake kiko tayari kwa mechi hiyo na wamejipanga kupata matokeo mazuri ili kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa.

Sven alisema kila mechi kwake ni muhimu na amewaandaa wachezaji wake kuiheshimu Gwambina kama walivyofanya katika michezo ya ligi hiyo iliyotangulia.

Alisema mechi zote ni ngumu na zenye ushindani, hivyo watacheza kwa umakini na tahadhari ili watimize malengo yao ya kuondoka na pointi tatu muhimu.

"Tuko tayari kwa mechi, tunatarajia itakuwa ngumu na yenye ushindani, kila timu tunajiandaa kwa ajili ya kupata ushindi, hatutarajii mechi rahisi, tena tunakutana na timu mpya kwenye ligi, ina wachezaji wanaohitaji kujitengeneza, hatutabweteka," alisema Sven.

Nahodha wa Simba, John Bocco aliliambia gazeti hili kila mchezaji wa timu hiyo atakayepata nafasi ya kucheza, amedhamiria kujituma na kutekeleza vyema majukumu atakayopewa.

Bocco alisema mechi zote kwao ni ngumu kwa sababu wao ni mabingwa watetezi ambao timu zote hujipanga kuwafunga na wao kuukaribia ubingwa.

"Hatuna mechi rahisi, kila mechi kwetu ni ngumu, hatutabweteka, malengo yetu ni kujituma na kucheza mpira wa kiwango cha juu na kuwapa furaha wanachama na mashabiki wetu," Bocco alisema.

Novatus Fulgence, Kocha Mkuu wa Gwambina FC alisema kwake mechi hiyo ni kama michezo mingine iliyotangulia ambayo ilikuwa migumu na yenye changamoto mbalimbali.

"Mechi zote ni ngumu, tumejiandaa na tumejipanga kupata pointi tatu, kikubwa ni wachezaji wangu kupunguza makosa, ukifanikiwa hapo na kutumia nafasi za kufunga vizuri, tutajiweka kwenye nafasi kubwa ya kupata ushindi, tunaamini katika soka hakuna timu ndogo," alisema Fulgence.

Aliongeza kwa kushirikiana na Mshauri wa timu, Mwinyi Zahera, wanaamini wataondoka na furaha katika mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 1: 00 usiku.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >